


MABIRIKA YAVUJAYO

 Na tuombe. Bwana, sasa tunaamini. Tunamwamini Mwana wa Mungu, na, kupitia jambo hili, tunaukubali Uzima wa Milele kwa Yeye. Sasa tumekutanika tena, aduhuri ya leo, ama jioni ya leo, kwa ajili ya ibada nyingine, tukikutumainia Wewe kwa ajili ya Ujumbe na kwa yale utakayotwambia usiku wa leo. Tunakuamini Wewe, Bwana, na kukungojea Wewe. Nawe ulisema, “Wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mbawa kama tai.” Nasi tunaomba, Mungu, ya kwamba utatupa hiyo Nguvu ya kupanda juu, usiku wa leo, tunapokungoja Wewe.

² Tunakushukuru kwa ajili ya watu hawa, na kwa yale wanayomaanisha Kwako na yale wanayomaanisha kwangu. Nakushukuru kwa ajili ya jambo hilo, Baba. Wao ni vito Vyako. Nami naomba, Mungu, ya kwamba usiku wa leo, ya kwamba utajidhihirisha Mwenyewe kwa njia, kwao, wanayohitaji. Iwapo kuna wagonjwa hapa, naomba waponywe. Kama kuna shaka katika nia ya mtu fulani; iondoe, Bwana. Na utupe tu Uwepo Wako na baraka Zako, kwa maana tunazihitaji, Bwana. Wewe ndiwe utoshelevu wetu wote. Pia, bila Wewe, hatuwezi kufanya neno.

³ Tunaomba ya kwamba Wewe utapokea shukrani zetu kwa yote uliyotenda. Katika Jina la Yesu Kristo tunatarajia baraka Zako. Amina.

Mwaweza kuketi.

⁴ Naam, vema, ni—ni baridi kidogo Jumapili hii usiku, humu, kuliko ilivyokuwa usiku wa Jumapili iliyopita. Tunawashukuru sana ndugu zetu waliofanya kazi kwa uaminifu sana kuleta hiki. Nawajua wawili au watatu wao. Ndugu Mike Eagan, kama ninavyomwona huko nyuma, nami. . . Ndugu Mike, na Ndugu Sothmann, Ndugu (naamini) Roy Roberson, na Ndugu Woods, na hao wote, walikuwa huku chini wakijitahidi sana, wakijaribu kuingiza kusudi tupate Ujumbe huu sasa, au leo. Kwa hiyo, tunashukuru.

⁵ Sasa, Jumapili ijayo asubuhi, Bwana akipenda, nataka kufanya ibada ya kuponya, maombi kwa ajili ya wagonjwa. Nasi tutaitenga kwa ibada ya kuponya, kama Bwana akipenda.

⁶ Niliona, asubuhi ya leo, kuna lundo la lesa hapa. Niliziomba. Nami, mlipokuwa mnaomba na kuimba, niliziomba hizi lesa; halafu kuna zingine hapa usiku wa leo. Kwa hiyo, tuna—tunaamini ya kwamba Mungu huwaponya wagonjwa. Shuhuda nyingi sana za kuponya miongoni mwetu, na duniani kote, nasi tunashukuru kwa jambo hili.

7 Nami niliwazia, Jumapili ijayo, kwa kuwa sina budi kuondoka kwa muda mfupi, nasi tumekuwa tukishikilia sana kufundisha na Ujumbe, hata nikawazia lingekuwa jambo zuri kama tulikuwa na—na ibada ya kuponya, tukawaombea wagonjwa. Nasi tunatumaini ya kwamba Mungu atatupa wakati mzuri sana.

8 Sasa, wengi wenu hamna budi kusafiri maili nyingi usiku wa leo. Kwa hiyo nilikuwa nikizungumza na makundi kule—kule kwenye Mkahawa wa Blue Boar, leo, mahali nilipokuwa nikila chakula cha mchana. Watu wengi wazuri, sina budi kuwasalimia na kuzungumza nao, watu ambao sijapata kukutana nao hapo awali, wanaokuja hapa kanisani. Nami ninashukuru kwa ajili ya marafiki kama hao, nami nataka kumshukuru kila mmoja wenu. Wengine wao wamechuma forsadi nyeusi, na kutuletea sisi. Na mmoja akatuletea ndoo ya asali, ama asali ya miwa, naamini ilikuwa ndiyo hiyo, na—na vitu tu. Hamjui hilo linamaanisha nini. Na asubuhi, naja huku na kutoka nyumbani, wakati mwingine kuna . . .

9 Asubuhi ya juzijuzi kulikuweco na ndugu pale ambaye alikuwa na hali mbaya sana, hakuwa na nguo na kadhalika, alitaka niende nikamletee nguo chache. Nikatoka, nami karibu niangushe ndoo ya forsadi nyeusi iliyowekwa pale, nikasema, “Je! wewe ndiwe uliyeleta hizi forsadi nyeusi?”

10 Naye akasema, “La, sihusiki kabisa. Nimekuwa hapa kabla ya mapambazuko, na zilikuwa hapa wakati huo.” Kumbe ni Ndugu yangu mwema Ruddell aliyeniletea hizo. Na, kwa hiyo, mambo hayo hakika nayathamini.

11 Billy Paul ndiyo kwanza anigusie, muda mchache uliopita, ya kwamba miongoni mwa kusanyiko hili usiku wa leo, wamekusanya matoleo, hayo kwa ajili yangu. Na—na nawashukuru kwa jambo hilo. Sikutaka mfanye hivyo. Na—nathamini jitihada zenu, na kadhalika, bali jambo hilo halikuwa la lazima. Na, hata hivyo, Bwana awabariki. Mwajua, mwajua, Biblia ilisema, “Kadiri mlivyomtenda mmojawapo wa hawa walio wadogo, mlinitendea Mimi.”

12 Sasa, nimekuwa nikizungumza nanyi kwa namna fulani, juu ya Ujumbe, waziwazi sana. Nami. . . Watu fulani huenda wakawa na wazo kwamba—kwamba mimi nadhani ya kwamba Yesu atakuja asubuhi ama usiku wa leo. Ndivyo ninavyodhani. Naam, sisemi ya kwamba Yeye atakuja. Na, tena, huenda Yeye asije hata juma lijalo, na huenda ikawa mwaka ujao, huenda ikawa miaka kumi. Sijui atakapokuja. Lakini, kuna jambo moja nataka ku- . . . daima mliweke mawazoni, mwe tayari kila dakika ama saa. Mnaona? Ili kwamba, kama hatakuja leo, huenda Yeye akawa hapa kesho. Kwa hiyo liwekeni hilo mioyoni mwenu, ya kwamba Yeye yuaja.

¹³ Na sijui ni wakati gani utakuwa muda wangu wa mwisho hapa duniani, wala hakuna mmoja wetu ajuaye. Na hakuna mmoja wetu ajuaye ni wakati gani Yeye atakapokuja. Hata Yeye hajui, Yeye Mwenyewe, kwa Maneno Yake Mwenyewe; Yeye alisema, “Baba, pekee, ndiye ajuaye Yeye atakuja lini; hata Mwana hajui Yeye atakuja lini.” Ni wakati Mungu atakapomtuma kwetu tena. Bali tunakutazamia Kuja Kwake. Na iwapo hatakuja katika kizazi changu, huenda akaja katika kile kijacho; kama hatakuja katika hicho, atakuja katika kile kifuatacho. Lakini, kwangu mimi, ni vigumu kuona wakati wo wote uliosalia. Mimi tu. . . Kwangu mimi, ingeweza kutukia dakika yo yote. Sasa, hilo halimaanishi. . . Hilo halimaanishi, sasa, ya kwamba utaona mbingu zikibadilika na kila. . . Huko siko kule kuja ninakozungumzia. Ninazungumzia kuhusu Kunyakuliwa.

¹⁴ Mnaona, anatumiza Kuja kutatu. Anakuja katika matatu ya Wana, Majina. Yeye alikuja katika utatu; Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Mnaona, yote hayo Kristo yeye yule, Mungu yeye yule, daima. Naam, tunajua alikuja kuleta kazi tatu za neema; kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kila kitu, katika Mungu, kinakamilishwa katika tatu-tatu.

¹⁵ Na kwa hiyo alikuja, mara ya kwanza, kumkomboa Bibi-arusi Wake. Anakuja, mara ya pili, kama Kunyakuliwa, kumchukua Bibi-arusi Wake. Anakuja, mara ya tatu, pamoja na Bibi-arusi Wake, Mfalme na Malkia; baadaye, hapo ndipo watu wengi wanakutarajia kule Kuja.

Bali anapokuja wakati huu, karibu hakuna mtu ye yote ila wale walio tayari watajua wakati ajapo. Kutakuweco na kukosekana kwa watu. Hawatajua kilichowapata. Wao watanyakuliwa tu, katika dakika moja, na kwamba watakosekana. “Watabadilishwa katika dakika moja, katika kufumba na kufumbua.” Kwa hiyo iweni tayari kwa ajili ya jambo hilo. Litakuwa jambo la kuchukiza hivi karibuni asubuhi kumkosa mpendwa, hakuna anayeweza kuwapata. Si ingekuwa vibaya sana kujua tayari kumepita nawe umekukosa? Kwa hiyo jiweke tu mbele za Mungu.

¹⁶ Naam, juma lijalo, Bwana akipenda, Jumatatu ijayo, juma moja kutoka Jumatatu hii, Mungu akipenda, nairudisha jamaa yangu huko Arizona ambako wao huenda shuleni, kisha ni—nitarudi.

¹⁷ Naam, siendi huko nje. . . Sina ibada zo zote za kuniweka huko. Ni vigumu kunipata Arizona. Huondoka nikaenda mahali pengine. Nitampeleka mke wangu kule, Jumatatu ijayo. Nitarudi tena hapa. Nitaondoka hapa nielekee British Columbia. Nitarudi Colorado. Nitakuwa Arizona tena inapokaribia Krismasi, kwa dakika chache tu, muda mrefu kutosha. . . labda siku mbili ama tatu, niikutanishe jamaa, nirudi huku inapokaribia sikukuu

ya Krismasi, Bwana akipenda, niwe na ibada kwenye juma la mwaka mpya hapa.

¹⁸ Kwa hiyo basi niko hapa, kwa kweli, mara nyingi zaidi. Niko hapa mara kumi zaidi ya ninavyokuwa kule, kwa maana hatuna kanisa lo lote wala ibada zo zote nje kule, hatuna cho chote huko nje, kwa hiyo, kwa namna ya ibada ya kanisa. Hilo ndilo jambo moja baya juu yake. Sina mahali pa kuwapeleka watoto ambapo watausikia Ujumbe huu, kama vile watoto wenu wanavyousikia hapa, na—na kwa hiyo huo ndio upungufu mmoja tulio nao. Bali wote wana afya nzuri zaidi. Hali ya hewa ni kavu, joto, kavu, lakini watoto wote wanaonekana wana afya nzuri zaidi. Sikai huko vya kutosha kujua kama pana afya ama hapa. Mimi, mimi situlii, na—na—nakisia nilizaliwa tu mzururaji.

¹⁹ Mke wangu huniita . . . Najua yuko hapa, kwa hiyo nitajuta jambo hili baada ya kanisa, nyote mwajua. Inaitwaje ile, pepo zinazohamahama, ama pepo zisizotulia, ama cho chote—cho chote kile, mwajua, mchanga wa kuhamahama? Ama, mimi daima situlii, kwa maneno mengine. Nami nimeoa sasa, miaka ishirini na miwili, nami wakati mwingine hufikiria ni mgeni hapo nyumbani, kwa maana sina budi kuondoka.

Bali ninautazamia wakati ambapo tutatulia katika ile Nchi ya uenyeji wetu siku moja. Bali sasa vita vimewaka moto, kwa hiyo na tuwe katika maombi.

²⁰ Msisahau, Jumapili ijayo asubuhi, Bwana akipenda, waleteni wagonjwa wenu na wanaoteseka. Njoni mapema, pateni nafasi, na labda kuna kundi litakolombewa. Hatuna budi kutoa kadi za maombi. Kama hakuna wa kutosha, hatutatoa kadi za maombi, za kutosha tu kuunda mstari mdogo wa kama dazeni mbili ama tatu, ama cho chote kile. Bali labda tu—tutatoa kadi za maombi, kwa hiyo labda tutafanya hivyo saa moja kabla ya ibada ya kawaida, ambayo nafikiri huchukua . . . itakuwa saa mbili, ama saa mbili na nusu, watatoa kadi za maombi; kufungua kanisa, kutoa kadi za maombi Jumapili ijayo asubuhi. Halafu hakikisha utakuwa hapa kwa ajili ya ninino yako . . . Waleteni wapendwa wenu, wawekeni mle. Itakuwa hali nzuri na ya baridi-baridi kanisani, kama wao ni wagonjwa, nasi tutafanya kila tuwezavyo kuwaombea.

²¹ Asanteni, tena, kwa matoleo ya upendo.

²² Na sasa tutasoma kidogo Neno la Mungu, usiku wa leo, na tuwe tayari kwa ajili ya tukio hili la Uwepo Wake tena kutuletea Neno Lake. Sasa, tunajua tunaweza kusoma fungu la maneno, bali Mungu hana budi kutufunulia maana yake. Mnaona? Tunaweza kuchukua fungu la maneno, bali Mungu hana budi kutufunulia maana yake. Na wakati mnafungua sasa katika Kitabu cha Yeremia, sura ya 2.

²³ Nataka kusema nafurahiwa kuwa, pamoja nasi, Ndugu Lee Vayle, ndugu mpendwa katika Bwana. Nami nafikiri hapa,

ndugu huyu hapa, siwezi kukumbuka jina lake, Ndugu Willard Crase. Tena nimewaona ndugu kutoka Arkansas, Ndugu John na wengineo, kutoka karibu na Poplar Bluff, na Ndugu Blair. Na, loo, Ndugu Jackson, na Ndugu Ruddell, na wengi sana ambao si—siwezi . . . Laiti ningalitaja jina la kila mtu, bali siwezi kweli, nanyi mwaelewa. Ndugu Ben Bryant, namwona ameketi hapa; yeye kwa kawaida ndiye kona yangu ya amina wakati nina- . . . Kila mtu anamjua Ben kwa sauti yake. A-ha.

²⁴ Sisi, tukiketi huko California wakati mmoja, nilikuwa ninawahubiri Wabatisti Ujumbe kule bondeni. Walikuwa na hema kubwa pale, na wengi wa Wabatisti wa tabaka ya juu. Sikuweza kusikia “amina” kutoka po pote; mwajua, wanaogopa baadhi ya hao wanawake wataharibu vipodozi nyusoni mwao. Halafu, muda si muda, nikaona miguu miwili imeinuliwa juu namna hiyo, ikiruka hewani, na mikono miwili mikubwa, na nywele nyeusi zikitikiswa pale, akipiga ukelele, “Amina,” akipaza sauti namna hiyo. Nami nikaangalia chini, nikasema, “Ben, ulitoka wapi?” Yeye kweli alikuwa akisema zile “amina.”

²⁵ Namwona mkewe akimwangalia, kidogo. Vema, yeye anapoteza kidogo-kidogo nywele hizo nyeusi, lakini hiyo ni sawa, mwajua. Usilijali jambo hilo. Nilipoteza, zangu, muda mrefu uliopita.

Kwa hiyo, sasa, msisahau kuomba.

²⁶ Sasa tunapofikia upande ulio wa unyenyekevu wa ibada, kumbukeni, kama tukilisoma Neno hili, basi Mungu atalibariki Neno Lake. “Halitamrudia bure, bali litatimiza kile ambacho limekusudiwa kwalo.” Nami najua, katika kulisoma Neno, daima nitakuwa sahihi. Ninapolisoma Neno, Mungu ataliheshimu Neno Lake.

²⁷ Sasa hebu tusimame kwa heshima ya Neno Lake. Yereimia, sura ya 2, aya ya 12 na ya 13 ya Yereimia 2.

E- . . . mbingu, staaajabuni kwa sababu ya jambo hili, mkaogope sana, na kuwa na ukiwa sana, asema BWANA.

Kwa maana watu wangu hawa wametenda maovu mawili; wameniacha mimi, niliye chemchemi ya maji ya uzima, wamejichimbia mabirika, mabirika yavujayo, yasiyo- . . . yasiyoweza kuweka maji.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

²⁸ Mungu mpendwa, Neno Lako limesomwa. Nasi tunaomba ya kwamba Wewe utaliheshimu Neno hilo na utupe leo mfano ama kifani Chake; huku tunapoangalia siku zilizopita, Israeli, kama mifano, kama Biblia inavyotufundisha ya kwamba tunaweza kuona uliyowatendea wakati walipolitii Neno, tuone ulivyowafanyia walipokosa kuliadini Neno, na tujue litupasalo kufanya. Kwa hiyo, tunaomba ya kwamba Wewe utanena nasi

usiku wa leo katika njia maalumu sana, tupate kujua jinsi ya kuenenda katika siku hii, ambayo tulijua asubuhi ya leo tunaishi. Kwa maana tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mnaweza kuketi.

²⁹ Nataka kuzungumzia usiku wa leo juu ya somo, kwa muda kidogo juu ya: *Mabirika Yavujayo*.

³⁰ Israeli walikuwa wametenda maovu mawili mabaya sana. Mungu alisema walikuwa wamemwacha Yeye, aliye Chemchemi ya Uzima, nao wamejichimbia mabirika ya kunywea. Sasa, hilo ni jambo fulani.

³¹ Sababu ya kufikiria juu ya somo hili ni kwa sababu lingeenda sambamba na yale niliyokuwa nikisema asubuhi ya leo, kuhusu saa tunayoishi, na Kile tunachoshindania.

³² Nasi tunawaangalia Israeli kama mfano, ambao, alichokuwa Mungu, Yeye daima amedumu yeye yule. Na kuna jambo moja tu ambalo Mungu aliwahi kuheshimu, hilo lilikuwa, njia Yake ambayo Yeye aliwaandalia watu. Na wakati walipoiacha njia hiyo, basi Mungu alitahayarishwa, naye Mungu akawafanya watu wajute kwa kuacha yale aliyowaambia watende, haidhuru ilikuwa nini.

Yeye hata aliwapa sheria, “Msiguse, msishike, msionje.” Si kwa sababu tu ya uovu wa kufanya jambo hilo, bali uovu wa kutotii yale aliyowaambia wafanye. Na daima hapawezi kuwepo na sheria bila adhabu ya sheria. Kwa maana, kama hakuna adhabu, basi, sheria haina maana sana isipokuwa iwe na adhabu. Hiyo sheria!

³³ Sasa, tunaona, waliyofanya katika siku hiyo yanaonekana yakienda sambamba na yale tunayotenda leo, yale wanayofanya watu wa kanisa.

³⁴ Sasa tunaona jambo geni hapa. Huenda likawa geni kwa watu wengine, wakati Yeye aliposema, “Ninyi, wao, wamejichimbia mabirika, mabirika yavujayo.” Sasa, labda wengi wenu hamjui birika ni nini. Wangapi wanajua birika ni nini? Vema, karibu ninyi nyote. Kama ulilelewa mashambani, unajua birika ni nini. Nakumbuka nimekunywa wadudu wa kutosha kwenye moja, ku—kujua bi—birika ilikuwa nini.

Nimehubiri kule mashambani ambako, kwenye miti ya vivuli, ambako ungepata mtungi uliojaa maji ya birika umewekwa pale, ya—ya mvua, mwajua, na kwa namna fulani yalika sana. Halafu wa—na halafu wadudu, wakati wa usiku, wangeingia mle. Na kwa hiyo najua maji ya birika ni nini.

³⁵ Bi—birika ni ma—mahali, kitu ambacho kimechimbwa ardhini, kuchukua mahali pa kisima. Mahali ambapo watu hawana kisima, basi wana bi—birika. Kwa maneno mengine, birika ni tanki lililojengwa na mwanadamu ama kisima kilichochimbwa na mwanadamu ardhini, ambacho mwanadamu

huchimba, kuyakinga maji, apate ku—kuyatumia. Wengine huyatumia kama maji ya kuoshea, na wengine huyatumia kama maji ya kunywa, na njia mbalimbali, labda. Maji yote wakati mwingine, ambayo tulikuwa tunayapata, yalikuwa ya birika. Tulikuwa na kitu cha kale ambacho ilikubidi kuzungusha, na kuzungusha, na kuzungusha, na kuzungusha, na kuzungusha, kuyavuta maji; kilifungiwa ndoo ndogo, kuyavuta maji hayo kutoka kwenye hilo birika.

³⁶ Vema, tunaona jambo moja ambalo birika linatofautiana na kisima. Naam, birika litakuwa tupu. Bi—bi—birika haliwezi kujijaza. Ni—ni . . . Halitumainiki. Huwezi kutumainia birika. Halina budi kutegemea na kuponea mvua ambazo hunya kwenye majira ya kiangazi ama kipupwe, yo yote ile ili . . . Kwa kawaida, majira ya kipupwe wakati theluji na mvua vinapoanza, basi huyaelekeza maji kwenye birika. Na iwapo halipati maji hayo, basi hu—huna maji kabisa. Yote—yote yanakauka. Na haliwezi kujijaza. Hilo birika la kale haliwezi kujijaza. Linajazwa na mvua—mvua inayonyesha.

³⁷ Nami nataka muone jambo jingine kuhusu birika. Kwa kawaida, mtaona, ama jinsi ilivyokuwa huko kwetu, birika . . . Kwa kawaida ghala ya nafaka ni karibu mara mbili ya nyumba, na kwa kawaida wao huyaelekeza maji hayo kutoka kwenye hicho kibanda, kwenda kwenye birika. Nakumbuka shimo hilo la birika ya kale kule, wakati yeye alipo- . . . wakati ma—mabomba ya kutolea maji yanaingia ndani yake, pia, nje ya hilo ghala la nafaka. Linajazwa toka kwenye lile ghala.

Basi hayo maji yanatolewa toka kwenye paa la hiyo ghala ya nafaka; ambapo, wanyama wote wanakanyaga—kanyaga kila mahali kwenye uwanja wa zizi, na kila taka ya uwanja wa kibanda hicho inakaa juu ya ile ghala ya nafaka, katika nyakati za kiangazi. Halafu maji yanakuja na kuifagia yote toka paani, yakaingia katika kihori ambacho ni cha kujitengenezea, kisha yakaingia kwenye mfuko wa maji wa kujitengenezea, mpaka kwenye birika la kujitengenezea. Na kama huna takataka, sijui una nini, unapokuwa na birika. Naam, bwana! Lote ni la kujitengenezea, na ni chafu kama iwezavyo kuwa.

³⁸ Mwajua, tulizoea kuiita . . . Tulikuwa na kitambaa cha kuchujia katika moja. Ulijua hicho kilikuwa nini? Ilitubidi kuweka kitambaa cha kuchujia juu yake, kuzuia wadudu wote na vitu vilivyotoka juu ya lile—lile ghala la nafaka, na kuzunguka mahali pale; na kuyamwaga kutoka mahali pamoja kuingia mahali pengine, hata kwenye birika. Nasi tulikuwa tunaweka ki—kitambaa cha kuchujia juu yake, kuzuia ta—taka zote za juu na kadhalika ambazo tuliweza. Bila shaka, hicho hakingaliweza kushika taka yenyewe, ilishika vitu vikubwa vilivyoshuka na kuliangukia. Huenda mdudu akaanguka mle ndani, bali utomvu wa mdudu huyo ulichukuliwa na maji. Kwa

hiyo, kwe—kweli ulikuwa na uchafu hapo ulipokuwa na birika chafu la kale.

³⁹ Katika siku chache, ukiacha maji hayo yakae pale, yanaoza. Ukiyaacha maji hayo yasimame kwenye birika, yanakuwa maji yaliyooza. Ndipo yanajaa—yanajaa vyura, na mijusi, na nyoka. Nasi tulizoea kuwaita “vifurukuta-mikia,” ninino wadogo. . . Sijui kama. . . Wao si kimelea, wao ni. . . Siwezi, sijui vile ungewaita. Bali vitu vidogo vinaingia majini, ambavyo tuliita vifurukuta-mikia. Mnajua ni nini. Wangapi wanajua ninachozungumzia? Loo, mbona, bila shaka, nyote mnaotoka mashambani mnajua. Mkiyafanya kuoza sana, na basi hawa wanaopenda maji yaliyooza wanaambatana nayo. Kwa kweli huja tu, kwa sababu maji yameoza. Na kwa sababu yameoza, yanawavutia wanyama mle wanaopenda vitu vilivyooza.

⁴⁰ Na hiyo ni kama makanisa yetu leo kabisa. Nafikiri ya kwamba tumeacha. . . Moja ya dhambi kubwa mno ambazo makanisa yametenda leo, kama Israeli wakati huo, yalimwacha Yeye, Chemchemi ya Maji ya uzima, na kujichimbia mabirika ya kujitengenezea. Nayo yanakuwa makao ya kila kitu kinachopenda maji ya namna hiyo. Mijusi, vyura, kwa maana ni tanki la kujitengenezea. Na katika tanki hili ambamo vitu hivi vinaishi, ni mfano mkamilifu wa madhehebu yetu leo.

⁴¹ “Sasa,” unasema, “Ndugu Branham, mbona unawashambulia sana watu hao?”

Wanapaswa kushambuliwa. Hawana budi kushambuliwa. Yatorokeni, kwa maana hatimaye yatafanyika ile alama ya mnyama. Kumbukeni, hilo ni Kweli! Yatakuwa ile alama ya mnyama. Madhehebu yataongoza moja kwa moja hata kwenye kitu hicho. Yamo njiani yakielekea kule sasa, kulazimisha, kwa kutumia nguvu.

⁴² Angalia kwenye himaya ya kale ya Kirumi. Jambo hilo ndilo hasa liliwaongoza kwenye ile alama ya ukengeufu. Mliona kwamba hapana mtu angaliweza kununua ama kuuza bila alama ya huyo mnyama. Ilimbidi kuwa nayo.

⁴³ Kuna tabaka mbili tu za watu watakaokuwa humu duniani; hao wenye Muhuri wa Mungu, na hao wenye alama ya mnyama. Tabaka mbili tu, kwa hiyo itakubidi kuwa na moja ama nyingine. Na itakuwa ukengeufu, a—alama ya—ya dini, dini kengeufu.

⁴⁴ Na itakuwa na alama ya mnyama. Tunaposoma, tunaona ya kwamba Rumi ilikuwa, ndivyo ilivyo, na daima itakuwa, ala- . . . ama, yule mnyama. Barabara. Hakuna njia ya kuipa cho chote kile. Rumi!

⁴⁵ Na Rumi ilifanya nini? Ilibadilika toka Rumi ya kipagani ikawa Rumi ya kipapa, kisha ikaunda madhehebu, madhehebu ya dunia nzima, ambayo yalimplazimisha kila mtu kujiunga na dini hiyo la sivyo atauawa.

46 Na ni jambo la ajabu ya kwamba hii Marekani inajitokeza jukwaani, nayo ni kama mwana-kondoo. Na mwana-kondoo ana pembe mbili ndogo, haki za kisiasa na za kidini. Na baada ya muda kidogo, wakati hiyo ilikuwa mwana-kondoo, tuliona kwamba ilinena kama lile joka na kutumia uwezo wote wa lile joka la kwanza kabla yake. Na Biblia inatwambia ya kwamba wao walisema, “Na tumfanyie sanamu yule mnyama.” Sanamu ni kitu mfano wa kitu kingine. Nasi tunaweza kuliona sasa hivi, katika hali yake ya ukengeufu, kanisa likiunda Baraza la Makanisa Ulimwenguni, ambalo ni sanamu ya nguvu za Rumi; na litawalazimisha watu kitu kile kile Rumi ya kipagani ilichowalazimisha. . . ama Rumi ya kipapa ilichowalazimisha. Kwa hiyo, hakuna njia nyingine, hakuna kitu kingine. Lakini hiyo ni Kweli.

47 Na hiyo ndiyo sababu ninayashambulia katika siku zangu, katika wakati wangu, kwa sababu hayana budi kushambuliwa. Ule mwito ulikuja, kwamba, “Tokeni kwake, enyi watu Wangu, msizishiriki dhambi zake!”

48 Naam, ninayinganisha hayo na haya mabirika machafu na yenye vinyaa. “Yeye Ndiye Chemchemi ya Uzima. Yeye Ndiye Maji ya uzima.” Nao watu wanayaacha hayo, na kujichambia mabirika ambayo yanaweza tu kuteka vinyaa. Hicho ndicho tu yanayoweza kuteka. Na hivyo ndivyo umadhehebu unavyofanya; unashika kila kitu kinachokuja na kinachotaka kujiunga nayo. Yako tayari kukichukua mradi kina pesa ama kinaweza kuvalia namna fulani. Haidhuru wao ni nani, wanatoka wapi, wanawachukua, hata hivyo.

49 Sasa tunaona, tena, ya kwamba, hii alama ya mnyama iliyoundwa hapa. Marekani, ni, nambari kumi na tatu. Ilianzishwa na koloni kumi na tatu. Ilikuwa na bendera iliyokuwa na nyota kumi na tatu, milia kumi na mitatu. Na hata inaonekana katika Ufunuo sura ya 13. Na Marekani daima imekuwa mwanamke, sanamu yake imo kwenye sarafu zetu. Hata kile kichwa cha Mhindi, kwenye peni, kina sura ya mwanamke. Tunajua jambo hilo, tunajua historia yake. Kila kitu, ile Kengele ya Uhuru, na cho chote kile, uhuru. . . Sanamu ya Uhuru ni, kwa kila hali, mwanamke. Mwanamke; nambari kumi na tatu. Mnaona? Sasa, ni—ni vizuri kuona mambo hayo.

50 Na sasa nimebashiri kwa ufunuo kutoka kwa Mungu, ama ono mnamo mwaka wa 1933, ya kwamba mambo saba yangetukia kabla ya wakati wa mwisho. Na ya kwamba, moja yao, kwamba, “Mussolini,” ambaye wakati huo alikuwa akianza kuwa dikteta, “atakuwa dikteta. Na, pia, yeye atafanya uvamizi na ashuke kwenda Ethiopia, naye angeitaka Ethiopia. Naye Roho, Yeye alisema, ‘Atajitumbukiza shimoni.’”

51 Sijui kama kuna ye yote wa watu wa kale ambaye amebaki katika Maskani haya, anayekumbuka nikisema kule katika

Ukumbi wa Redman huku chini tulipohubiri, miaka mingi, mingi sana iliyopita. Yupo mmoja humu jengoni, usiku wa leo, ambaye amesalia kutoka wakati ule kule kwenye Ukumbi wa Redman nilipohubiri jambo hilo, wakati N.R.A ilipojitokeza, huko nyuma kabisa katika kipindi cha kwanza cha Roosevelt? Nakisia hakuna mmoja humu ndani aliyesalia. Yupo? Naam, naam, mmoja, kuna mmoja. Naam, Bibi Wilson, namkumbuka. Mke wangu, anayeketi kule nyuma. Wamesalia wawili, kutoka kizazi hicho cha kale cha watu hao katika siku hiyo.

Hapo, wakati wao walisema ya kwamba hii N.R.A. ilikuwa ndiyo alama ya mnyama, nikasema, “Hakuna cha hiyo; hata kidogo. Alama ya mnyama haiji hapa. Inatoka Rumi. Na haiwezi kuwa alama ya mnyama.”

⁵² Na sasa kumbuka ya kwamba mambo haya yalisemwa. Kasema, “Adolf Hitler atafikia kikomo chake kisichofahamika. Naye angetangaza vita dhidi ya Marekani. Nao wangejenga kitu ki—ki—kikubwa mno cha saruji, ya kwamba hata wataishi ndani yake. Na papo hapo Wamarekani watapigwa vita vibaya sana, mahali hapa.” Nayo ilikuwa ile boma ya Siegfried, miaka kumi na mmoja kabla hata haijaanza kujengwa. Kisha nikasema, “Bali atafikia mwisho wake; na Marekani itashinda hivyo vita.”

⁵³ Kisha nikasema, ya kwamba, “Kuna itikadi tatu; Unazi, ufashisti, na ukomunisti.” Ndipo nikasema, “Zote zitaishia kwenye ukomunisti. Urusi utazichukua zote, katika ukomunisti.”

⁵⁴ Basi nikasema, “Ndipo sayansi itafanikiwa sana, mwanadamu atakuwa mwerevu sana, hata atavumbua vitu vingi sana hata ataunda motokaa ambayo ina umbo la yai, ambayo itakuwa na kitu kama glasi upande wa juu, na itaendeshwa na nguvu zingine mbali na usukani.” Nao wana hiyo motokaa.

⁵⁵ Ndipo nikasema, “Kisha uadilifu wa wanawake wetu utashuka katika mambo ya aibu sana, hata watakuwa aibu kwa mataifa yote. Watavaa nguo za wanaume. Wataendelea kuvua nguo zao hata kweli wafikie mahali ambapo wana nguo zao za ndani tu, hivyo tu. Na, hatimaye, watafikia kuvaa tu jani la mtini.”

Na kama ukiangalia, katika toleo la mwezi jana la gazeti la *Life*, walikuwa na mwanamke aliyevalia jani la mtini. Na hiyo ni ile teitei ya jioni, ama gauni, kile wanachovaa jioni; inaona, waweza kuona kilicho ndani, ni majani ya mtini ambayo yanaficha tu sehemu fulani ya miili yao; na bila ukanda, ama na ukanda, nguo za kuogelea zisizo na ukanda, upande wake wa juu, yuko uchi. Na jinsi mambo hayo yametendeka!

⁵⁶ Kisha nikasema, “Nilimwona mwanamke amesimama Marekani, kama malkia mkuu ama kitu fulani. Naye alikuwa na sura nzuri, bali katili moyoni. Naye akalifanya taifa lipige hatua, lifuate nyayo zake.”

⁵⁷ Kisha nikasema, “Hatimaye, akaniambia niangalie Mashariki tena. Basi, nilipofanya hivyo, niliona, ilionekana, kama kwamba, ulimwengu ulikuwa umelipuka. Na umbali nilioweza kuona, hapakuweko na kitu ila vijiti, na—na mawe yanayowaka na kufuka moshi yalikuwa yamelipuliwa kutoka ardhini.”

Na haya yalikuwa yatendeke kabla ya mwisho wa dunia. Na matano ya yale saba tayari yametukia, katika miaka thelathini na mitatu. Haya basi, tumerudi katika wakati wa mwisho!

⁵⁸ Nami nikanena dhidi ya huo utaratibu wa kimadhehebu papo hapo. Nami ningali ninaamini, usiku wa leo, ya kwamba ni mahali palipojaa maovu, ya kwamba ni mahali ambapo vinyaa hutiririkia. Siwezi kuamini ya kwamba Mungu kamwe angeweza kuingiza kitu kama hicho Kanisani Mwake, kwa maana hakina budi kuzaliwa kwa Roho wa Mungu kisha kiohwe kabla hakijaitwa Chake. Mwili wa siri wa Kristo, sote tumebatizwa ndani Yake kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu.

⁵⁹ Naam, utaratibu huu wa birika bila shaka ni mfano mkamilifu wa madhehebu. Mtu mwenye hekima anapaswa kutahadhari, na asiye akaingia mle, kwa maana Mungu amethibitisha katika nyakati zote ya kwamba Yeye anayapinga na hajafanya kazi nayo kamwe. Kundi lo lote. . . Wakati wo wote mtu alipoinuka na ujumbe, kama vile Luther, Wesley, ama kadhalika, na Smith, na Calvin, na wengineo; walipounda madhehebu, Mungu alikiweka kitu hicho rafuni na kamwe hakukizuru tena katika ufufuo.

⁶⁰ Chunguza historia. Hapajakuwepo na wakati ambapo Mungu alichukua madhehebu, akafanya ufufuo kwake, hakuna mahali po pote. Basi, katika historia na kwa Biblia, inathibitika kwamba hicho ni kitu kichafu mbele za Mungu, kwa hiyo sitaki uhusiano wo wote nacho. Na hiyo ndiyo sababu mimi napinga. Ninajaribu kuwatoa watu mle.

⁶¹ Tumealikwa, kama vile katika Israeli, ndivyo ilivyo na sasa, kuiangalia Israeli tupate mifano. Wao, maadamu walidumu na Chemchemi ile, walikuwa sawa. Bali walipoanza kujichimbia wenyewe mabirika, taratibu za kujitengenezea, basi Mungu akawaacha kabisa. Atatufanya vivyo hivyo. “Wamemwacha Yeye, Chemchemi ya Maji ya uzima.” Hayo ndiyo malalamiko aliyokuwa nayo Mungu dhidi yao. “Kufanya kitu ambacho wao wangeweza kusema, ‘Mnaona kile tumefanya!’”

⁶² Sasa, katika wakati wa sa—safari ya Musa; wakati Mungu, kwa neema, alikwishawapa nabii, alikwishawapa ile Nguzo ya Moto iwatangulie, akaithibitisha kwa ishara na maajabu. Neema ilikwishatoa mambo haya yote. Israeli bado walitaka, waliona sheria. Waliikataa neema, wakachukue sheria.

Hivyo ndivyo watu wanavyofanya leo hasa. Wanalikataa Neno, kuchukua taratibu ya kimadhehebu, kwa maana katika

hayo wanaweza kufanya wanayotaka kufanya na bila kizuizi. Bali huwezi kufanya jambo hilo katika Kristo. Huna budi kuwa msafi na mweupe, kusudi uwe ndani ya Kristo.

⁶³ Wanakiacha kisima kinachofoka maji, wakaziendea taratibu za kujitengenezea ama birika, ungeweza kuwazia mtu fulani akifanya hivyo? Ungewazia jinsi ilivyo akili ya mtu ambaye angekunywa maji matamu ya kisima kinachofoka maji, kisha ayaache hayo akanywe ya birika la kujitengenezea lenye vyura, na mijusi, na vifurukuta-mikia, na kila kitu.

Hata halionekani kuwa jambo la busara kuwa sawa, bali hilo ndilo hasa watu wamefanya. Wao wameliacha Neno, Chemchemi ya kweli ya chanzo cha Nguvu za Mungu, kunywa maji ya mabirika, na kujitengenezea mabirika. Kama vile walivyofanya wakati huo, ndivyo wafanyavyo sasa. Wanasema . . .

Yeye alisema, “Wao wameniacha Mimi.” Hapa Yeye alisema, hapa katika Yeremia 2:14, ama 13, hasa. Yeye alisema, “Wameniacha Mimi, Niliye Chemchemi ya Maji ya uzima.”

⁶⁴ Naam, tunaona birika ni nini. Tunaona inachokinga. Tunaona jinsi inavyotengenezwa. Ni kitu cha kujitengenezea ambacho hutoka kwenye paa iliyo chafu. Yale maji yanayomwagika chini, hugonga kwenye paa lililo chafu, kisha yanatiririka tu kutoka kwenye paa, yanapitia kwenye kihori cha kujitengenezea, yanapitia kwenye mfuko wa kujutengenezea yakaingia katika tanki la kujitengenezea. Na vinyaa vyote vinarundikana mle, na vi-viini, na mijusi, na vyura, na vitu vya ardhini, hupenda hayo. Pia, tazama, wao ni wanyama walio wachafu; vifurukuta-mikia, maji yaliyooza. Kifurukuta-mkia hakiwezi kuishi katika maji masafi. Kama kikiishi, yatakiva. Hakina budi kuwa katika maji yaliyooza.

⁶⁵ Na hivyo ndivyo ilivyo na vingi vya hivi vimelea leo. Hamwezi kuishi katika maji mazuri ya Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo sababu wao wanapinga Neno kwa dhati, na kusema, “Linajipinga. Halifai kitu.” Ni kwa sababu hawana budi kuwa na kitu kama kidimbwi chenye maji yaliyooza kufurukutia mle. Sawa.

Hivyo ndivyo ilivyo kwa vyura, na kwa mijusi, na viluwiluwi, na vitu kama hivyo. Hawana budi kusogea kwenye bwawa ama kidimbwi chenye maji yaliyooza, wapate kuishi, kwa maana asili yao ni kuishi mle. Na huwezi kumbadilisha mnyama huyo mpaka uibadilishe asili yake.

Wala huwezi kumfanya mtu alione Neno la Mungu mpaka asili yake imebadilishwa; na wakati asili yake imebadilishwa kutoka alivyo, akawa mwana wa Mungu, na Roho Mtakatifu anaingia ndani yake. Roho Mtakatifu aliliandika Neno la Mungu!

⁶⁶ Leo nilikuwa nikizungumza na rafiki yangu mwema, Daktari Lee Vayle, ambaye yupo sasa. Naye ni mwanatheolojia

halisi, na kwa hiyo sisi kwa kawaida huwa na—huwa na maongezi mazuri juu ya Maandiko. Ana akili sana.

Basi aliniuliza wakati mmoja vile nilivyofikiria juu ya ushahidi wa kwanza wa Roho Mtakatifu, “Ulikuwa ni kunena kwa lugha?” Ndivyo imekuwa miaka mingi iliyopita.

Nikasema, “La; siwezi kuona hilo.”

Yeye akasema, “Wala mimi nami,” kasema, “ingawa nimekwishafundishwa jambo hilo.” Akasema, “Unafikiri ushahidi wake ni nini?”

⁶⁷ Nikasema, “Ushahidi kamili kabisa ninaoweza kufikiria ni upendo.” Na kwa hiyo tukaingilia kuzungumzia jambo hilo.

Na kwa hiyo nikawaza ya kwamba hilo lilionekana zuri sana kwa hiyo nikashikilia hilo tu, “Kama mtu ana upendo.”

Bali siku moja Bwana, katika ono, akanisahihisha. Naye akasema, ya kwamba, “Ushahidi wa Roho ulikuwa ni wale ambao wangeweza kulipokea Neno,” wala si upendo, wala kunena kwa lugha, bali ni kulipokea Neno.

⁶⁸ Halafu basi Daktari Vayle alikuwa akiniambia, ya kwamba, “Hilo ni Maandiko,” akasema, “maana, katika Yohana 14, Yesu alisema, ‘Wakati Yeye Roho Mtakatifu atakapowajilia, atawafunulia mambo haya, ambayo nimewafundisha, naye atawaonyesha mambo yajayo.’”

Kwa hiyo huo hapo ushahidi halisi wa Roho Mtakatifu! Yeye hajaniambia bado jambo lo lote ambalo si sahihi. Ya kwamba, “Ni ushahidi wa Roho Mtakatifu, ni yeye yule anayeweza kuliadini Neno, kama unaweza kulipokea.”

Maana, Yesu hakusema kamwe, “Roho mtakatifu akiisha kuja, mtanena kwa lugha.” Yeye hakusema kamwe, Roho Mtakatifu akiisha kuja, mngefanya yo yote ya mambo hayo. Lakini Yeye alisema, “Yeye atachukua mambo haya yaliyo Yangu na kuwapasha habari, na mambo yajayo atawapasha habari zake.” Kwa hiyo huo hapo ushahidi halisi wa Roho Mtakatifu, kulingana na Yesu Mwenyewe.

⁶⁹ Kwa hiyo hisi hizi zote na kadhalika walizo nazo watu na wangali wanaishi kwazo, mnaweza kuona kwa nini wanafanya hivyo. Unaona, inakuwa madhehebu, ama kidimbwi chenye maji yaliyooza, na hakuna madhehebu yatakayoundwa juu ya... Neno kamilifu la Mungu. Haiwezekani, kwa maana huwezi ukachagua ama kuunda madhehebu kutokana na Mungu. La, bwana!

⁷⁰ Sababu yake ni kwamba, unalipata kundi la watu wanaoweza kuliadini Neno, acha waunde madhehebu. Muda si muda, katika mwaka mmoja kuna kundi la akina Ricky mle ndani ambao hungeweza kutenda kitu nao. Wameshika hatamu, nawe huwezi kufanya kitu juu yake. Si mpango wa Mungu. Si wa Mungu, kwa hiyo tunajua kitu hicho hakifai kitu. Kinakuwa

birika, na kinakuwa mahali ambapo kila mmoja atapatana katika jambo *hili, lile*, ama *lingine*, kuwaingiza washiriki mle, ama kuwaacha watu waingie.

⁷¹ Tunaona, utaratibu huu ulianza wakati mmoja, kule nyuma katika siku za Israeli, wakati walipokuwa wakichimba mabirika haya. Na kulikuweko na mtu mmoja na kundi la Mafarisayo ambao walikuwa wamechimba mabirika machache. Nao walikuwa na mtu jina lake Herode, naye alikuwa mtangazaji, liwali wa huo mkoa.

Basi akashuka akaja kumsikiza mtu fulani ambaye hakuchezacheza na madhehebu yao. Yeye alikuwa nabii. Na hakuna nabii aliyekuwa na uhusiano wo wote na madhehebu, bali aliyachukia. Huyu nabii akaanza kusema, “Msianze kusema ndani yenu, ‘Baba yetu ndiye Ibrahimu,’ kwa maana nawaambieni Mungu anaweza kumwinulia Ibrahimu watoto katika mawe haya.”

⁷² Nao wakamleta mtu mashuhuri kumsikiza. Na mtu huyu mashuhuri alikuwa amemnyag’anya ndugu yake mke, na akamwoa. Basi huyo mtu alisemaje alipoenda mbele yake? Wao walifikiri atapatana, na kusema, “Naam, bwana, wewe, karibu kwenye kiti kizuri hapa. Nawe yakupasa ku- . . . Ninashukuru sana kwamba umekuja huku kunisikiliza leo.”

Yohana alienda moja kwa moja mbele yake, akasema, “Si halali kwako kumchukua.” Jambo la kwanza kabisa alilosema, alimkemea kwa ajili ya dhambi yake.

⁷³ Unaona, madhehebu hutengeneza vidimbwi vilivyooza ambamo mwanamume anaweza kuishi na wanawake, na hao wanawake anaweza kufanya yasiyofaa, na kukata nywele zao, na kuvaa kaptura, na cho chote kile, na kujiita Wakristo.

Bali chemchemi halisi, haleluya, ya Uweza wa Mungu, haiwezi kukaa pale, kwa maana inaisukumia nje. “Mimi Ndimi Chemchemi ya Maji ya uzima.” Waliniacha Mimi, kujichimbia baadhi ya mabirika.”

⁷⁴ Sasa, chemchemi ya maji ya uzima, tunaona, chemchemi ya maji ya uzima ni nini? Tumeona birika ni nini, basi chemchemi ya maji ya uzima ni nini? Ni kisima kinachofoka maji.

“Kisima kinachofoka maji, ni kitu gani hicho, Ndugu Branham?”

Ni kisima ambacho sikuzote hutoka huko chini na kusukuma maji yake yatoke nje. Daima yanatiririka. Kinajitegemea chenyewe. Daima ni matamu na masafi, kisima kinachofoka maji, chemchemi ya maji ya uzima. Hayajakufa na kuoza. Yanaishi, yanabadilika kila wakati, yakitoka kitu kipya wakati wote, yakiendelea, yakitoka kwenye vyanzo vyake. Yanatoa nguvu zake kutoka—kutoka kwenye chanzo chake, ambacho ni . . . bado ni chemchemi ya maji ya uzima

yakinyunyizia. Kinajisafisha chenyewe; ni maji masafi na matamu. Kinajitegemea; si lazima ungojee mvua kulijaza tanki. Daima kinafurika, kinatoa maji yake bure. Si lazima uyavute kwa mashine, kuyavuta kwa winji, kuyavuta, ama kujiunga nayo. Ni chemchemi tu ya maji ya uzima.

⁷⁵ Mnajua, mkichukua mabirika haya ya kale, huna budi kuyazungusha, na kuyazungusha, na kuyazungusha kwa mpini, kuyavuta kwa mashine na kila kitu, kusudi upate kuteka maji kidogo ya hayo yaliyoza. A-ha!

Bali Chemchemi ya Maji ya uzima huyatoa, bure, bila kuyavuta kwa mashine, kujiunga, cho chote kile. Loo, ninashukuru kwa ajili ya Chemchemi hiyo! Naam, bwana!

⁷⁶ Haihitaji kutiwa kichujio, kuwatoa vimelea. Kwa maana, ina kina kirefu sana, mle kwenye Mwamba, mpaka hamna vimelea mle.

Haihitaji kuning'iniziwa tambara la kielimu, hiyo ni kweli, mipango iliyotengenezwa na ulimwengu ya hekima ya kimadhehebu ya kujitengenezea; kukwambia, mbele ya daktari wa bongo, kama unaweza kuhubiri au la. Haining'iniziwi moja ya hayo matambara yaliyotiwa unajisi. Ingezisukumia mbali mara unapozitia mle. Huwezi ukafanya jambo hilo. Hicho kisima kinabubujika, kila wakati. Kama ukikivalisha moja ya hayo matambara, kingeyatupilia mbali upande mmoja au mwingine. Hakina wakati wa kuvalia matambara ya kimadhehebu.

⁷⁷ Hakihitaji chujio, hakihitaji kichujio, hakihitaji kuvutwa kwa mashine, kushtuliwa ghafla, wala cho chote kile. Kiko pale tu, kinabubujika. Si lazima kitegemee mvua ya mahali pale ili kijae. *Mvua* ni "fufuo." Wapi? Chemchemi ile, ni hapo penye Chemchemi ya Uzima. "Palipo na mzoga, tai watakusanyika." Haikubidi kuvuta ufufuo kwa mashine; haikubidi kuvuta cho chote kwa mashine. Jambo tu likupasalo kufanya ni kuja kwenye ile Chemchemi. Daima imejaa maji mazuri na matamu, nayo haikomi. Hububujika tu daima.

⁷⁸ Si lazima uende kwenye birika, na kusema, "Vema, kama ikinyesha na maji yatiririke kwenye lile ghala la nafaka, tutapata maji ya kunywa." Mnaona? Jamani, jamani! Si hiki. Kisima hicho kinachofoka maji, daima kinabubujisha maji mazuri na baridi. Unaweza ukakitegemea. Si lazima useme, "Vema, nitaondoka niende kwenye hili birika la kale. Tulizoea kunywa maji mle, bali mvua haijanyesha muda mrefu. Nakwambia, huenda ikawa limekauka."

⁷⁹ Hivyo ndivyo zilivyo baadhi ya taratibu hizi za kujitengenezea. Unaweza kuingia mle, kama unendeleza kitu fulani kikubwa, kama una shirika fulani kubwa la kisiri la kuuza vitu, ama—ama namna fulani ya kitu kinachoendelea, na karamu kubwa na kadhalika vikiendelea, michezo ya anasa, na

karamu katika orofa ya chini, na kila kitu, huenda ukaipata nyumba imejaa.

Lakini unapoenda mahali ambapo Chemchemi hiyo inabubujika, kila mara, watu wako pale wakipata kinywaji cha maji mazuri na baridi. Unaweza kuitegemea! Useme, “Hawajapata ufufuo kwa miaka kumi”? Kama unaishi karibu na Chemchemi hiyo, sikuzote ina ufufuo unaoendelea.

⁸⁰ Kama alivyosema maskini yule Muwelshi. Ama, wakati mmoja wakati ufufuo wa Kiwelshi ulikuwa unaendelea, kulikuwa na watu mashuhuri kutoka Marekani. Madaktari wengi wa Elimu ya Kiungu walikwenda Welshi, kutafuta ni wapi na kuna nini. Kwa hiyo walikuwa na kosi zao zilizopinduliwa, na kofia zao zenye kizibo, nao walikuwa wakishuka kwenda barabarani.

Basi huyu hapa maskini polisi anakuja, akiizungusha fimbo yake ndogo mkononi mwake, huku anapiga mruzi, “Pale msalabani alipofia Mwokozi wangu, hapo nililia nipate kusafishwa na dhambi; hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu, Jina Lake litukuzwe,” huku anatembea barabarani.

Kwa hiyo wakasema, “Huyu anaonekana kuwa mtu wa dini. Tutaenda kumuuliza.”

Nao wakasema, “Bwana!”

Kasema, “Naam, bwana?”

Akasema, “Tumekuja hapa kutoka Marekani. Sisi ni wajumbe. Tumekuja hapa kuchunguza ufufuo wa Kiwelshi, kama unavyoitwa. Sisi ni Madaktari wa Elimu ya Kiungu, na tuko hapa kuuchunguza.” Akasema, “Tunataka kujua mahali ulipo huo ufufuo, na mahali unapofanyika.”

Akasema, “Bwana, mmekwishafika. Mimi ndimi ufufuo wa Kiwelshi.” Amina! “Ufufuo wa Kiwelshi umo ndani yangu. Umo humu.”

⁸¹ Hivyo ndivyo ilivyo unapoishi karibu na ile Chemchemi ya Maji ya uzima. Hayo ni hai sikuzote, yakibubujika na kububujika, kububujika na kububujika. Hayaishi. Si eti, “Nenda kaangalie kama maji, kama tulipata mvua hapa muda mrefu uliopita,” si hivyo. Ni Chemchemi hiyo ya Maji ya uzima. Kama nilivyosema, inatoa Maji yake bure.

⁸² Si lazima uivike matambara, upate kujua; nguo fulani za kielimu, kabla hujamtuma nje akahubiri, na kuona kama anaendeleza maneno yake sawa, anayatamka sawa, kama anatumia majina na vijina vyake sahihi, na kadhalika, na visifa. Wengi wao hata hawajui hivyo ni nini, lakini anaishi kwenye ile Chemchemi hata hivyo, mnaona, vivyo hivyo.

⁸³ Si lazima itegeemee mvua ya mahali hapo, kuijaza, ama ufufuo wa mahali hapo, kwa ajili yake. Si lazima ifanye hivyo, kwa maana Nguvu zake na usafi wake vimo ndani yake. Humo

ndimo lilimo Neno, Nguvu Yake Yenyewe! Mtu anapoweza kulipokea moyoni mwake, ina usafi Wake. Ina nguvu Zake. Iko katika Neno Lenyewe, inafoka Uzima.

⁸⁴ Kila Israeli walipoiacha, walipata taabu. Kila walipoiacha, walipata taabu.

Ndivyo tunavyofanya leo. Wakati ufufuo unapoondoka kwenye Hiyo, basi haufai kitu. Unajichimbia visima vichache, na, ama mabirika yenye maji yaliyooza, na basi umekwisha.

⁸⁵ Bali Yeye sikuzote aliwasaidia. Kule kunung'unika pale kwenye Bahari Shamu, ndipo waliponung'unika . . . Hata hivyo, katika hayo yote, Yeye alikuwa amewaahidi, amewapa ahadi. Angewarudishia papo hapo, jinsi tunavyoliangalia; bali alikuwa ameahidi kuwapeleka kule.

Yeye alifanya nini? Hao wana wa Israeli, aliwapa ile Nguzo ya Moto na kila kitu, kwa ajili ya uthibitisho, nabii wao. Nao wakawaongoza kule nje hadi baharini. Na, daima, kuna shida juu Yake. Basi hapa Farao anakuja na jeshi lake. Basi unajua alilofanya Mungu? Aliifungua tu hiyo birika nyekundu, yenye maji yaliyooza.

Bahari ya Chumvi ndicho kitu kilichokufa kabisa zaidi ya vyote ulimwenguni. Kweli imekufa. Ina maji yaliyooza. Hamna kinachoweza kuishi ndani yake.

Basi akaifungua na kuwaweka huru, ng'ambo ya pili. Akawachukua mahali ambapo haitawalazimu kufungwa na kitu kama hicho.

⁸⁶ Kule jangwani, waliona ya kwamba matanki hayangetegemewa; yalikuwa yamekauka. Waliona kwamba, walitoka katika shimo moja la maji hata kwenye lingine. Walipokuwa kule jangwani, walikuwa wanakufa njaa, kwa maji ya kunywa. Nao wangeliliendea hili tanki hapa, dimbwi la maji; lilikuwa limekauka. Wakaondoka wakaenda mahali pengine; pamekauka. Hawangefikiri kabisa watapata maji ya kunywa.

Ndipo basi katika mahali pasipoelekea kabisa katika jangwa lote, wakayapata maji. Yalikuwa katika mwamba. Yalikuwa katika mwamba. Mahali pasipoelekea kabisa ambapo mtu angepata maji, pangekuwa katika mwamba uliokauka katikati ya jangwa. Lakini, mnaona, Mungu hufanya mambo namna hiyo. Katika mahali pasipoelekea kabisa, katika njia isiyo ya kawaida kabisa. Hayo ndiyo tumekuwa nayo sikuzote.

⁸⁷ Wao wanafikiri huna budi kuyakusanya madhehebu makubwa, pamoja, na uyaache yote yakusanyike pamoja na shughuli nyingi huku na huko, na kadhhalika, na kuwashirikisha maelfu, na wote namna *hii*, kufanya ufufuo.

Wakati mwingine Mungu humchukua maskini jamaa mdogo ambaye hata hajui ABC zake, na miongoni mwa watu wasiojua

kusoma ambao ni vigumu kupambanua kati ya mkono wao wa kulia na wa kushoto, Yeye anaweza kuinua ufufuo ambao utautikisa ulimwengu. Yeye alifanya hivyo katika wakati wa Yohana. Alitenda hivyo katika wakati wa manabii. Hakuna hata mmoja wao, tujuavyo sisi, aliyepata kuwa na elimu, lakini Mungu angeweza kuwachukua na kufanya jambo fulani nao.

⁸⁸ Katika Mwamba huu yalitoka maji. Yeye alikuwa ndiye ule Mwamba. Naye akauamrisha huu Mwamba, nao hauna budi kupigwa. Naye akampa kila mtu aliyetaka kunywa wingi wa maji masafi, matamu, na mazuri. Yeye aliwaokoa wote waliokunywa Kwake. Jambo hilo linaenda sambamba kabisa na Yohana 3:16.

*...Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa
Mwanawe pekee, ...kila amwaminiye asipotee, bali
awe na uzima wa milele.*

⁸⁹ Mungu aliupiga huo Mwamba, pale Kalvari. Hukumu yetu ilikuwa juu Yake, ili kwamba kutoka Kwake aje Roho wa Uzima ambaye angenipa mimi na wewe Uzima wa Milele. Huo ni mfano mkamilifu Wake, hapa jangwani.

⁹⁰ Haikuwalazimu kuvuta, kuchimba, kuvuta, ama cho chote kile; wanashiriki tu katika njia aliyoiandaa Yeye, bure. Ambapo, haikuwalazimu kuivuta juu toka kwenye dimbwi la maji. Haikuwabidi kuyavuta juu kwa ndoo. Haikuwabidi kuwa na winchi kuyateka. Iliwabidi tu kuyanywa.

Na hivyo ndivyo ilivyo leo. Haikubidi kujiunga na cho chote. Haikubidi kupiga magoti madhabahuni na kuanzisha jambo fulani, kuvuta. Haikubidi kurudiarudia neno, hata unapata mchafuko wa lugha. Jambo tu likupasalo kufanya ni kumnywa Yeye, bure, njia iliyoandaliwa na Mungu. Hakuna kuvuta, hakuna kusukuma, hakuna kitu; ichukue tu, bure. Haikulazimu kufanya kitu; Mnywe tu. Hiyo ni kusema, mwamini Yeye tu. Hayo tu ndiyo niwezayo kusema juu yake.

Haikuwalazimu kufanya jambo lo lote juu yake. Haikuwalazimu kuchimba wayapate. Haikuwalazimu kupiga magoti na kulia usiku kucha, kwa ajili yake. Waliyanywa tu; ulikuwa umepigwa na ukawa tayari. Hiyo ni kweli.

⁹¹ Ninamwangalia mtu fulani sasa, ameketi huko nyuma ya chumba hiki hapa. Nakumbuka nilipomwambia hilo, kwenye zizi la ghala la nafaka la kale siku moja, karibu na hori.

Naye akasema, “Lakini mimi sifai.”

⁹² Nikasema, “Najua hufai.” Kisha nikasema, “Wala mimi sifai, pia.” Bali nikasema, “Unaangalia ulivyo wewe. Basi acha kuangalia ulivyo wewe, ukaangalie alivyo Yeye.”

Akasema, “Laiti ningaliweza kuziacha hizi sigara, Ndugu Branham, ni—ni—ningekuwa Mkristo.”

93 Nikasema, “Usiziache. Unajaribu kuwa mzuri kisha uje Kwake. Yeye hakuja kuwaokoa watu wazuri; alikuja kuwaokoa watu wabaya waliojua wao ni wabaya.”

Akasema, “Vema . . .”

Nikasema, “Sikiza, hutaki kwenda jehanamu, sivyo?”

Akasema, “La.”

94 Nikasema, “Vema, haikubidi kufanya hivyo. Yeye alikufa kusudi isikubidi kwenda.”

Akasema, “Inanipasa kufanya nini?”

Nikasema, “Hakuna. Ni rahisi tu namna hiyo.”

Yeye akasema, “Bali kama nikiweza tu . . .”

95 Nikasema, “Huyoo, unarudia habari za sigara tena. Acha kuwazia juu ya sigara hiyo. Kumbuka tu, wazia juu Yake, yale aliyofanya, kile alichu Yeye; si kile ulicho. Wewe si mwema; na hujakuwa mwema, na kamwe hutakuwa mwema. Lakini, kile alichu Yeye, Yeye Ndiye!” Nami nikasema, “Sasa, jambo pekee likupasalo kufanya; kama Yeye alipachukua mahali pako kule chini, wewe tu kubali kwa hiari yako yale aliyofanya. Jambo likupasalo kufanya tu ni kulikubali.”

“Mbona,” akasema, “hilo ni rahisi. Nitafanya hivyo.”

96 Nikasema, “Hiki hapa kijito.” Mnaona? Nikampandisha nikamleta hapa na kumbatiza katika Jina la Yesu Kristo.

Baadhi ya watu wake wameketi hapa, nami—nami najua walijisikia vinginevyo nilipofanya hivyo, bali nilijua nililokuwa nikifanya. Niliona katika mtu huyo kitu kilichokuwa halisi. Ningeweza kukiona mle, nami nikamchukua na kumbatiza katika Jina la Bwana Yesu.

Na, tulipofanya hivyo, haikuwa muda mrefu baadaye nikaenda nyumbani kwa mwanawe wa kiume. Tuliona o—ono la mti ukivunjwa mahali fulani, na mtu huyo akaanguka, nusura auvunje mgongo wake. Akapelekwa hospitalini. Ndipo usiku huo Bwana akanifunulia, mimi, kwamba huo ulikuwa ndio mwisho wa hizo sigara.

Kwa hiyo kesho yake alitaka sigara. Nikasema, “Nitamnunulia katoni moja nimpelekee. Ngoja utaona, siku zake za sigara zimekwisha.” Yeye hajawahi kuvuta moja tangu wakati huo, na hajataka moja tangu wakati huo. Mungu!

97 Mnaona, jambo la kwanza likupasalo kufanya ni kuja kwenye Chemchemi ile. Huna budi kuja kwenye Maji hayo, utambue si kitu ambacho wewe unaweza kufanya. Ni yale Yeye aliyokutendea. Haikubidi kuchimba; haikubidi kuyavuta; haikubidi kuacha *hiki*; haikubidi kuacha *kile*. Jambo likupasalo kufanya tu ni kwenda kule na unywe. Hayo tu. Ikiwa una kiu; kunywa!

⁹⁸ Sasa, Yeye alikuwa ule Mwamba. Mungu alimpiga kwa ajili yetu, Naye akatoa wingi wa maji masafi na matamu. Angali anayatoa, leo, kwa ye yote ambaye ataamini. Hii ni neema Yake, bila shaka, kwa watu Wake, sisi.

⁹⁹ Kuna kitu kama pale, kama watu wa siku hizi, wako tayari kupokea wanachoweza kupata, bali hawataki kutoa huduma kwa ajili yake. Israeli walikuwa tayari ku—kuunywea ule mwamba sasa, bali hawakutaka kumtolea Mungu huduma aliyostahili.

¹⁰⁰ Na Yeye daima anatumia. Mnajua, hata hatuwezi kupumua bila Yeye. Hatuwezi kupumua bila huduma ya Mungu. Hivyo ndivyo tunavyomtegemea. Na, hata hivyo, karibu ituvunje vipande viwili kama tukijaribu kufanya, kumtendea Yeye kitu fulani. Yeye anatumia kufanya jambo fulani, tutoke twende tukamwone mtu fulani, tukamwombee mtu fulani, tukamasaidie mtu fulani, karibu lituvunje moyo, kufanya jambo hilo. Lakini hatutaki kumtolea huduma yo yote.

¹⁰¹ Malalamiko yake yalikuwa, “Wameniacha Mimi, Neno; nao wamekubali birika livujalo, badala yake. Wamekubali. . . Wameniacha Mimi, Niliye Chemchemi ya Uzima, Chemchemi ya Maji ya Uzima; nao wanatamani na wanaona afadhali kunywea birika yenye maji yaliyooza.” Ungeweza kuwazia jambo hilo?

¹⁰² Ungeweza kuwazia mtu sasa, ambaye, hiki hapa kisima kinachofoka maji kikitoa hayo maji mazuri, yatokayo kwenye mawe ya chokaa, yakitoka moja kwa moja toka katikati ya miamba, huko chini kwenye fungu la mchanga, na kadhalika, baridi tu na mazuri yawezavyo kuwa; na anaona afadhali anywee birika iliyo kule, ambayo yalikuwa yametiririka kutoka juu ya ghala ya nafaka, na kwenye zizi, na vibanda vya nje karibu na mahali hapo? Na kuyaweka kwenye birika hilo pale, ambapo maji yanayopenya huchuruzikia mle, kutoka kwenye ghala ya nafaka, na maboma na mazizi, na kila kitu kikichuruzikia kwenye hilo birika, halafu tunataka kuku-. . . tungenywea hilo kabla hatujaenda kwenye hicho kisima kinachofoka maji? Mtu huyo angekuwa na kasoro bongoni. Hiyo ni kweli.

¹⁰³ Na wakati mwanamume ama mwanamke atachukua msimamo wa madhehebu, yatakayoruhusu kukata nywele, kuvaa kaptura, vipodozi, kila namna ya hivi vitakataka vingine, na namna fulani ya m—mpango, na kufanya mambo haya yote yasiyofaa, na anaweza kwenda kwenye mchezo wa matufe, na—na upuzi huu wote kule, na anaweza kuvumilia mambo hayo; na kupenda hayo vizuri kuliko wanavyolipenda Neno la Mungu la mtindo wa kale ambalo hukata na kuchimba, na kuwafanya wanawake mabibi, na linawachukua na kuwafanya wavalie vizuri na kuenenda vizuri, linaondoa sigara na tumbaku, na kuapa na kulaani, na kudanganya na kuiba, mbali nawe, na ulimwengu wote kukutoka, na likakupa Kitu

ambacho kinaridhisha kabisa. Kwa nini wewe mwanamume ama mwanamke unakiendea kitu kama hicho ati upate faraja? Waweza kupata faraja kwa kitu hicho?

¹⁰⁴ Waweza kupata maji mazuri kutoka kwenye birika lenye maji yaliyooza? Mtu anawezaje? Kama mtu akienda kwenye birika la maji yaliyooza kupata maji ya kunywa, wakati tayari kuna kisima kinachofoka maji, ungesema, “Mtu yule ana kasoro bongoni.”

Na kama mwanamke ama mwanamume akienda mahali kama hapo kupata faraja, huyo mtu ana kasoro ya kiroho. Hawalitaki Neno. Inaonyesha ya kwamba asili yao ingali ya chura, ama kiluwiluwi, ama cho chote kile, hiyo ni kweli, kitu cha asili hiyo kinachopenda kidimbwi hicho chenye maji yaliyooza, kwa maana vitu vya aina hiyo havitaishi katika kidimbwi cha Maji masafi. Haviwezi kuishi; ni Maji masafi. Haviwezi kuishi.

¹⁰⁵ Naam, malalamiko yalikuwa, “Wameiacha.” Na leo wamefanya jambo lile lile.

Sasa angalia yule mwanamke kisimani. Vema, alikuja kwenye birika la Yakobo, naye alikuwa anateka maji pale wakati wote, kwenye birika la Yakobo. Lakini birika la Yakobo, madhehebu, tungeyaita maana alichimba matatu; na hili alilochimba. Sasa, yeye alikuwa na hadithi kubwa. Yeye alisema, “Naam, baba yetu alichimba kisima hiki, Yakobo. Yeye alikinywea, na ng’ombe zake zikakinywea, na kila kitu. Si hayo yatosha?”

¹⁰⁶ Yeye akasema, “Lakini maji unayochota humo, unaona kiu tena, inakubidi kurudi hapa na kuyateka tena. Lakini,” kasema, “Maji nikupayo wewe ni Chemchemi, Chemchemi ya maji yanayoruka juu sana yakibubujika kutoka ndani, nawe hutakuja hapa kuyateka. Yamo pamoja nawe.”

¹⁰⁷ Angalia. Lakini alipoona kwamba Chemchemi ya Kimaandiko imemzungumzia, kwa ishara ya Kimaandiko ambayo alikuwa akiitazamia, aliiacha hiyo taratibu ya kimadhehebu ya Yakobo na hakurudi mle tena, kwa maana alikuwa ameupata ule Mwamba halisi. Mnaona? Akaenda mbio mjini. Alikwisha acha dhambi. Hakuwa mwanamke mchafu tena. Alisema, “Njoni, mtazame Mtu niliyempata, Mtu aliyeniambia mambo niliyoyatenda. Je! haimkini Huyu ndiye Kristo?” Yeye...Huenda birika hilo lilikuwa sawa; lilikuwa limetimiza kusudi lake. Sasa yeye alikuwa kwenye ile Chemchemi ya kweli. Lile birika lilikuwa sawa mpaka ile Chemchemi ya kweli ilipofunguliwa. Lakini ile Chemchemi ya kweli ilipokuja, hilo birika likapoteza nguvu zake. Akaona kwamba kuna mahali pazuri zaidi pa kunywea.

¹⁰⁸ Na kuna mahali pazuri zaidi. Kuna mahali pazuri zaidi, na hapo ni katika Kristo. Katika Yohana Mtakatifu 7:37 na 38, Yesu

alisema, katika siku ya mwisho ya sikukuu ya vibanda, “Mtu akiona kiu, na aje Kwangu, anywe.”

Wote walikuwa wakifurahi. Walikuwa na mbubujiko mdogo wa maji yakitoka chini ya madhabahu, na—nao wote walikuwa wakinywea huo, katika sherehe, ya—ya ile sikukuu. Ndipo akasema, “Baba zetu waliunywea mwamba wa roho jangwani.” Mnaona, walikuwa wamejichimbia birika, maji yaliyooza waliyoyavuta kutoka mahali fulani, na kuyabubujisha mle chini ya hekalu pale. Nao wote wangepazunguka maji haya wakayanywa, na kusema, “Miaka kadha iliyopita, baba zetu walinywea jangwani.”

Yesu alisema, “Mimi Ndimi Mwamba ule uliokuwa jangwani.”

Kasema, “Tulikula mana kutoka Mbinguni, Naye Mungu akainyesha.”

¹⁰⁹ Kasema, “Mimi Ndimi Mana hiyo.” Yeye, Chemchemi ile, alikuwa amesimama miongoni mwao. Hicho Chakula cha Uzima kilikuwa kimesimama miongoni mwao.

Na hata hivyo hawakukitaka. Waliona afadhali wawe na birika lao; kwa sababu, mwanadamu alikuwa ameitengeneza *hii*, Naye Mungu alikuwa ameituma Ile. Hiyo ndiyo tofauti yake hasa. Wakajichimbia mabirika!

¹¹⁰ Yeye alisema, “Mtu akiona kiu, na aje Kwangu, anywe.” Yeye Ndiye Chemchemi ile.

Na kama vile Maandiko yalivyosema, “Mito ya Maji yaliyo hai itatoka ndani yake.” Loo, Yeye ni kisima kinachofoka maji! “Kutoka ndani yake, au utu wa ndani kabisa, itatoka mito ya Maji yaliyo hai.”

¹¹¹ Yeye ndiye Mwamba ule uliokuwemo ndani, uliokuwa mwamba wa Hajiri, katika wakati wa shida; wakati mtoto wake alipokuwa karibu kufa, wakati alipokuwa amefukuzwa kambini, naye alikuwa kule nje na mtoto Ishmaeli. Maji yake, katika birika lake alilokuwa amebeba, yalikuwa yamekwisha. Naye akamlaza mtoto Ishmaeli chini; akaondoka akaenda, kadiri ya mtupo wa mshale, akalia, na, loo, kwa sababu hakutaka kumwona huyo mtoto akifa. Mara, Malaika wa Bwana akanena, naye akapata Bia-Sheba, kile—kile kisima kilichokuwa kinabubujika, na kingali kinabubujika hata leo. Yeye alikuwa Beer-Sheba wa Hajiri, mwamba kule jangwani.

¹¹² Ilikuwa imesimama hapa katika Chemchemi iliyojaa Damu, siku ile, ikisimama pale hekaluni. [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] . . . wakati wa tufani. Katika Zekaria sura ya 13, Yeye alikuwa ile Chemchemi iliyofunguliwa katika nyumba ya Daudi, kwa kusafisha, na kwa (dhambi) kusafishwa dhambi. Yeye alikuwa Chemchemi hiyo. Na katika Zaburi 36:9, Yeye

alikuwa Chemchemi ya Uzima ya Daudi. Yeye yungali ni Chemchemi ile katika nyumba ya Daudi.

Naye ni wa yule mshairi, moyoni mwake pale, mshairi alisema:

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotoka kwenye mishipa ya Imanueli,
Wenye dhambi wakitumbukizwa ndani ya
mafuriko hayo,
Hupoteza mawaa yao yote ya hatia.

Yeye ndiye Chemchemi hiyo ya Uzima, Chemchemi ya Maji. Yeye ni Neno la Mungu.

¹¹³ Watu wa siku hizi za mwisho wamemwacha Yeye, Neno la kweli, Maji ya Uzima; nao wamejichimbia mabirika ya kimadhehebu; na, tena, wakachimba, walichimba!

¹¹⁴ Na sasa tunaona ya kwamba, wanayo yanayovuja, walikuwa na mabirika yanayovuja. Halafu birika hili limejazwa viini visivyoamini, kujigamba kusikoamini, miradi ya elimu, na kadhalika, ambayo haiambatani na ahadi za Mungu. Wao ni wanaoshuku Neno.

¹¹⁵ Sasa, mabirika haya waliyo nayo, Biblia ilisema, yalikuwa “yanavuja.” Birika *linalovuja* ni birika “linalomwaga maji,” na yanapenyea nje. Yanafanya nini? Yanapenyezea mahali pa kidini palipojaa maovu panapoitwa Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Na hapo ndipo birika linalovuja linapowaongoza, kwa sababu tu wao wamemwacha, na wame. . . Chemchemi ya Maji ya uzima; na kujifanyia mabirika haya.

¹¹⁶ Wanachimba miradi mikubwa ya seminari ya masomo, elimu, na kadhalika. Hayo ndiyo aina ya mabirika wanayochimba leo, kwamba mtu hana budi kupata Ph.D., ama LL.D., ama Shahada ya Sanaa, ama cho chote kile, kabla hajaenda kuhubiri. Mabirika ambayo yamejaa theolojia ya kujitengenezea. Wao wanawapeleka katika shule hizi kubwa mno za masomo, na humo wanawadunga kwa theolojia za kujitengenezea, na kuwatuma na hizo. Ni siku ya namna gani tunayoishi, mabirika ya kujitengenezea! Hapana shida. . . Si ajabu kitu hicho kimekuwa ha—harufu mbaya, loo, jamani, ni kwa sababu watu wananywea hayo.

¹¹⁷ Na watu wanapotaka kujifurahisha leo, wanafanya nini? Watu, badala ya kuikubali furaha ya Bwana, wanaigeukia dhambi, wapate furaha. Watu wanaokwenda kanisani na kudai kwamba ni watumishi wa Kristo, wanaposhikwa na wasiwasi sana huwasha sigara. Na wakati wao—wakati wao wanataka ku—kujifurahisha, wanavaa nguo zao chafu na kutoka nje wakakate nyasi wakati wanaume wanapita, kusudi wawafanye wawapigie mruzi. Wanafanya cho chote kile wapate kupendwa na watu. Wao wanataka kuonekana kama wacheza sinema mashuhuri. Hiyo ndiyo furaha yao.

Wakati, Yesu alisema, “Mimi Ndimi niwatoshelezaye.”

Sababu ya wao kuendea jambo hilo, ni kwa sababu hawataki kuinywea Chemchemi hiyo. Wameikataa. Hawataki kuinywea. Wamejiunga na namna fulani ya taratibu za kujitengenezea, namna fulani ya birika iliyojaa namna zote za vitu vilivyooza, waweze kwenda hivyo.

¹¹⁸ Jana, tuliwapeleka watoto huko mtoni, ama naamini ilikuwa Jumamosi asubuhi. Tulishuka kwenda; Billy alikuwa anavua samaki kwa boti. Nasi tukapanda tukaenda na watoto, mjukuu wangu mdogo na wengineo, binti yangu, na mwanangu mdogo, nasi tukaenda upande wa juu wa mto ku—kuendesha boti. Hata hungeendesha boti mtoni, kwa ajili ya watu wenye vinyaa, wachafu, waovu sana huko mtoni, nusu uchi na wakifanya yasiyofaa. Boti moja ilikuja karibu nasi, kundi la wavulana wenye umri wa miaka kumi na miwili, kumi na minne, kila mmoja ana kopo la pombe mkononi mwake, na sigara. Wanakuita huko “kujifurahisha.” Loo, jamani! Ulimwengu huu unaweza kudumu muda gani, ukiwa na utaratibu kama huo?

¹¹⁹ Kisha ili kujiepusha na mawazo kwamba watakapokufa wataenda kuzimu, jambo wanalofanya, wanaondoka wanaenda na kujiunga na mabirika haya ya kujitengenezea. Kwa hiyo watu wa aina hiyo ni washiriki wa birika hilo. Si kitu ila kundi la vifurukuta—mikia vichafu, na vyenye vinyaa vya ulimwengu. Nao wanajishirikisha kwa jambo hilo kwa maana, kama alivyozoea kusema mamangu mzee, “Kila ndege na wimbile.” Hawatakuja kwenye ile Chemchemi wapate kusafishwa na maisha hayo ya dhambi. Wao wanataka kuishi kule nje, na waendeleo kushikilia ushuhuda ya kwamba wao ni Wakristo. Kwa nini? Wamemwacha, Chemchemi ya kweli ya furaha, Uzima, Maisha makamilifu na ya kuridhisha. Hilo ndilo kusudi lao la kufanya hivyo, kwa sababu wanataka kujiunga. Wana namna ya watu kule wanaoamini upuzi kama huo.

¹²⁰ Hapa si muda mrefu uliopita, mimi na Ndugu Fred, na Ndugu Tom, baadhi yetu tulikwenda kuhudhuria kanisa maarufu la Kibatisti katika mji wa Tucson, kuona kama tusingepata kitu fulani kidogo ambacho labda kingetuburudisha kidogo. Basi yule muhudumu akasema kitu fulani kuhusu watu huko Misri, walipoondoka walikuwa wakila vitunguu saumu na kadhalika, walitaka kurudi tena wakale hivyo. Kasema, “Hivyo ni kama walivyo watu siku hizi.”

Basi, sisi, kila mmoja akasema, “Amina!” Sijapata kuona kundi kama hilo! Kanisa zima likaaacha kumwangualia mhubiri likiangalia nyuma kuona ni nani aliyesema “amina.” Liliwaogopesha nusura wafe. Hawakujua ilikuwa ni nani.

Wakati, Daudi aliposema, “Mpigieni Bwana kelele za shangwe. Msifuni kwa vinubi! Msifuni kwa kinanda! Kila mwenye punzi na amsifu Bwana! Nanyi msifuni Bwana!”

Mungu hufurahi katika watu Wake. Hebu na wale waliofunzwa, waseme, “Amina,” wakati lo lote limesemwa sawa.

¹²¹ Mbona usiache utaratibu huu na mabirika ya ulimwengu, uingie kwenye utaratibu mwaminifu wa Mungu, ambao ni kisima kinachofoka maji, Yesu Kristo? Mbona usimgeukie, ambapo Mungu ndiye atupaye wingi wa furaha yetu, ndiye atupaye wingi wa sifa, ndiye atupaye wingi wa uradhi wetu. Kutulia kwa neva zangu hutoka kwa Mungu.

Wakati nimehuzunika sana, napata uradhi wangu katika Kristo, si katika sigara, si katika mambo ya ulimwengu, si katika kujiunga na baadhi ya kanuni za imani, lakini katika kumpata Yeye, Neno lililoahidiwa ambalo Yeye alisema, “Kama nikienda, nitakuja tena na kuwapokea.” Napata furaha yangu katika jambo hilo. Yeye Ndiye Furaha yangu.

¹²² Wao wanasema leo, kwa kujiunga na mambo haya na kuunda hili Baraza la Makanisa la Ulimwenguni, ya kwamba watatengeneza mahali pazuri zaidi pa kuishi. Kwa maoni yangu maaminifu, watatengeneza mahali pazuri zaidi pa kutendea dhambi. Hiyo tu ni . . . Kitu hicho chote ni dhambi, hata hivyo; si pa kuishi, bali pa kutendea. Kufanya mahali pake pa kutendea dhambi—kutendea dhambi, badala ya pa kuishi.

¹²³ Kitu kingine cho chote nje ya Yesu Kristo na Neno Lake la Uzima ni birika linalovuja. Kila kinachojariibu kuwa badala Yake; kila unachojariibu kufanya kukuletea amani, kila unachojariibu kufanya kukupa faraja, kila namna ya furaha unayopata kutoka kitu kingine cho chote, kama kibadilisho cha Huyu, ni birika linalovuja lililojaa vinyaa. Yeye anatoa uridhi mkamilifu.

¹²⁴ Nakumbuka hapa, majira machache ya kiangazi yaliyopita, nilitokea mlango wa nyuma. Kulikuweco na kijana mlaghai mamboleo kule nje aliyeniambia, kasema, “Wajua, sababu ya wewe kuzungunza juu ya wanawake namna hiyo, kuvaa hizo kaptura na kadhalika,” akasema, “ni kwamba wewe ni mzee.” Kasema, “Hiyo ndiyo sababu yake.”

Nikasema, “Angalia hapa. Una umri gani?”

Kasema, “Ishirini na saba.”

¹²⁵ Nikasema, “Nilipokuwa mdogo kuliko wewe kwa miaka mingi, nilihubiri jambo lile lile.”

Nilipata Chemchemi yenye kuridhisha. Yeye ndiye fungu langu. Amina! Mradi anajazi hayo, uzuri ndio huo. Huo—huo ndio ninino yangu. . . Huo ndio ustadi wangu, ni kumtazama Yeye, kuangalia kazi ya mikono Yake na kuona kile anachofanya. Sijui chemchemi nyingine!

Loo, huo ni mtiririko wa thamani
 Unaonifanya mweupe kama theluji;
 Sijui chemchemi nyingine,
 Ila Damu Yake Yesu.

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
 Iliyotoka kwenye mishipa ya Imanueli,
 Ambapo wenye dhambi wakitumbukizwa
 ndani ya mafuriko hayo,
 Hupoteza mawaa yao yote ya hatia.

¹²⁶ Nawaambieni, sijui chemchemi nyingine ila Chemchemi hiyo. Ilinisafisha nilipokuwa mchafu. Inaniweka msafi, kwa sababu nataka kuishi Mle, nipate kunywa haya Maji matamu yanayojaza nafsi yangu furaha.

Hata naweza nikawa nimeshushwa moyo sana, na kujisikia kwamba ni vigumu kwangu kuendelea, zamu nyingine, siwezi kwenda mahali pengine; ndipo naweza kupiga magoti na kuweka kidole changu kwenye ahadi, na kusema, “Bwana Mungu, Wewe Ndiye nguvu zangu. Wewe Ndiye uniridhishaye. Wewe Ndiwe yote katika yote kwangu.” Naweza kuanza kusikia Kitu fulani kikibubujika kutoka ndani yangu pale. Natoka ndani yake.

¹²⁷ Kwa kuwa nishapita umri wa miaka hamsini, ninaamka asubuhi, mnajua jinsi ilivyo, ni vigumu kwako kuutoa huo mguu mmoja kitandani. Jamani, ni vigumu kufanya hivyo; na mtu fulani yuko mlangoni, anapiga hodi, ama Billy akiniambia kuna jambo la dharura, mahali fulani ninapopaswa kwenda. Nami nawazia, “Nawezaje kufanya hivyo?” Najaribu kuutoa mguu mmoja nje.

Nawazia, “Wewe ni Chemchemi iliyojaa nguvu zangu. Amina! Nguvu zangu na msaada wangu hutoka kwa Bwana, Wewe ndiye kisima changu kinachofoka maji! Wewe ndiwe ujana wangu! ‘Hao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mbawa kama tai; watapiga mbio, wala hawatachoka; watakwenda kwa miguu, wala hawatazimia.’ Bwana Mungu, hili ni jukumu langu, kwenda. Nimeitwa kwenye wajibu wangu.” Na muda si muda, Kitu fulani kinaanza kuchemka ndani yangu.

¹²⁸ Juzijuzi, huko katika mahali padogo, nilikuwa na mkutano kule Topeka, Kansas; akatokea kijana, muhubiri mdogo, mmoja wa wadhamini wangu wa kwanza. Ndugu Roy, anayeketi hapa, anapakumbuka mahali pale. Katika mahali hapa, katika mahali hapa mashuhuri pale, palikuwa na m-... Huyu mhudumu alikuwa ameingia chini ya paa ama mahali fulani, ukuta wa kando ukamponda chini yake. Maskini kijana huyo alikuwa anakufa. Ini lake limepasuka. Wengu wake ulikuwa umegongwa ukatolewa mahali pake. Tani kadhaa zilimwangukia.

¹²⁹ Niliketi kwenye kiamshakinywa, nikizungumza na mke wangu. Nikasema, “Mke wangu, unajua, kama Yesu angalikuwa hapa, unajua Yeye angefanyaje?” Nikasema, “Wakati alinidhamini, naamini Neno hilo, alikuwa akimdhamini Kristo.” Kisha nikasema, “Hiyo ni hila ya ibilisi.” Nikasema, “Kama Yesu angalikuwa hapa, angeenda amwekee mikono Yake mitakatifu. Huyu kijana angepona. Sijali kama ini lake limepasuka. Angepata afya, kwa maana Yesu angeingia mle akijua Yeye alikuwa ni nani hasa. Yeye alijua wito Wake, Maandiko yalikuwa sahihi, yakithibitisha ndani Yake kwamba Yeye alijua alikuwa nani, na si. . . hapana shaka yo yote. Yeye angemwekea mikono Yake, na kusema, ‘Mwanangu, upate afya,’ aondoke pale.” Kisha nikasema, “Hakuna pepo wa kutosha kuzimu kumuua kijana huyo, wakati huo.” Nikasema, “Yeye angepata afya.” Lakini nikasema, “Unaona, mpenzi, Yeye alikuwa Yesu, mikono mitakatifu ya Mungu.”

Nikasema, “Mimi ni mwenye dhambi. Nilizaliwa kwa kujuana kimwili. Baba yangu na mama yangu pia walikuwa wenye dhambi, nami ni bure na safai kitu.”

Kisha nikasema, “Bali unajua nini? Kama Mungu angenipa ono na kunituma kule, basi hilo lingekuwa jambo lingine.” Nikasema, “Ningeshuka niende nimwekee mikono yangu, angetoka kwenye hicho kitanda kama Yeye alinipa ono.”

¹³⁰ Ndipo nikaanza kufikiri, “Hata hivyo, kama ilikuwa ono, ilikuwa nini? Ni mikono ile ile michafu juu yake, a-ha, mtu yule yule akimwombea, mikono ile ile michafu.”

Kisha nikaanza kuwazia, “Mimi ni mwakilishi Wake. Basi, Mungu hanioni mimi. Damu Hiyo ya Mtu Yule mwenye haki iko pale madhabahuni; inaniombea mimi. Yeye ndiye anayenitosheleza. Yeye ndiye maombi yangu. Yeye ndiye Uzima wangu.” Nikasema, “Jambo pekee ambalo lingenifanya nimwekelee mikono, kwa imani, ni kwa sababu nilikuwa na imani katika lile ono. Na bila ya ono, imani ile ile ingefanya jambo lile lile; kwa hiyo najihesabu mimi si kitu, bali namhesabu Yeye kuwa yote katika yote kwangu. Yeye Ndiye Uzima wangu. Yeye Ndiye aliye niagiza. Hakuna madhehebu yaliyonituma; Yeye alinituma. Haleluya! Naenda katika Jina Lake. Nitaweka mikono juu yake.” Nikashuka nikaenda kule nikamwekelea mikono kijana huyo, na usiku huo alikuwa katika mkutano, mzima kabisa. Amina!

¹³¹ Loo, ndiyo, Yeye ndiye ile Chemchemi. “Sijui chemchemi nyingine. Ila Damu Yake Yesu!” Mimi ninanuka, mimi ni laghai, kila mmoja wetu ndivyo alivyo, bali mbele za Mungu sisi ni wakamilifu. Ye. . . “Kwa hiyo iweni wakamilifu, kama Baba yenu aliye Mbinguni alivyo mkamilifu.” Unaweza kuwa mkamilifu? Kwa maana Aliye mkamilifu anatuwakilisha kule. Hiyo Chemchemi iko kila siku, safi. Si kitu fulani kilichooza,

bali safi kila siku, ambayo husafisha dhambi zangu zote. Yeye ndiye Chemchemi hiyo.

¹³² Sasa katika kufunga, ningesema hivi. Kila kilicho tofauti na Hiki ni mabirika yavujayo, na hatimaye yatamwaga yale utakayotia ndani yake; kama unaweka matumaini yako yote, wakati wako wote, na kila kitu, katika moja ya hayo mabirika yaliyoza. Yesu alisema ya kwamba yalikuwa mabirika yavujayo. Mungu alisema, “Yanavuja, yatamwaga cho chote unachotia ndani mwao.” Huwezi kuendelea mbele zaidi nayo, kwa maana yatamwaga cho chote unachotia ndani. Kwa maana Yeye ndiye njia pekee ya kuelekea kwenye ile Kweli, kwenye Uzima, hata furaha ya Milele, na amani ya Milele. Yeye ndiye tu peke Yake na njia pekee ya kwenda Kule. Loo, jamani!

¹³³ Chemchemi ya Uzima isiyokauka ni Yesu Kristo. Kwa nini? Naye ni Nani? Neno, yeye yule; Neno, Uzima, Chemchemi, “yeye yule jana, leo, na hata milele.” Kwa mwamini wa kweli, Hiyo upeo wa furaha yake, upeo wa Uzima wake. Na upeo wa uradhi wake uko katika Kristo. Hakuna cha kuvuta kwa mashine, hakuna cha kuvuta, hakuna cha kujiunga, hakuna cha kuteka; ni kuamini tu na kustarehe. Hivyo ndivyo alivyo kwa waaminio.

¹³⁴ Kama vile baba Ibrahimu; yeye hakuvuta kamwe, hakuhangaika, hakufadhaika. Yeye alikuwa na Neno. Aliyalalia matiti ya El Shadai. Wakati Ibrahimu alipokuwa na umri wa miaka mia moja, Mungu alimtokea, akasema, “Mimi Ndimi Mwenyezi.” Neno la Kiebrania ni *El Shadai*, maana yake, “Mwenye Matiti.” “Nawe u mzee, na nguvu zako zimekwisha, lakini kaa kifuani Mwangu unyonye nguvu zako toka kwenye Chemchemi hii.” Amina! Alinyonya hata akapata nini? Mwili mpya. Alimpata mtoto, kwa Sara. Na, miaka hamsini baadaye, alipata watoto saba kwa mwanamke mwingine.

¹³⁵ Loo, El Shadai! Agano la Kale linaonyesha alivyofanya, Agano Jipya linasimulia atakayofanya. Amina. Katika Agano la Kale. . .

¹³⁶ Sasa hewa haibaridishwi, kwa hiyo nitaharakisha na kuachia hapa sasa, katika dakika moja.

Ningetaka kusema jambo hili kabla sijafunga. Nilikuwa na mfano mzuri wa jambo hili wakati mmoja. Nilikuwa nikilinda wanyama. Na watu wengi hapa, huko chini karibu na Georgetown, huko chini katika Milltown, kulikuwa, huko mbali sana vilimani, na chemchemi. Ilikuwa ni kisima kinachofoka maji. Kingeyarusha nje, mkondo wa maji wa yapata fu—futi nne ama tano, yalichuruzika wakati wote, na pakawa na chemchemi kubwa mno pale. Na kila mahali kuizunguka kulikuwa na mirehaha hii hapa mingi, mwajua, vitu hivi vinavyokua hapa, kama mnanaa. Na, loo, nilikuwa nikitamani sana kwenda kule, loo, jamani, kufikia hiyo chemchemi. Nami ningelala tu karibu

na kitu hiki nikanywa na kunywa, kisha nikaketi na kunywa, nikangoja.

Na mwaka baada ya mwaka ningali ningekuja kwenye chemchemi ii hii. Haikukauka kamwe, kipupwe ama kiangazi. Hawangaliweza kukigandisha. Huwezi kukigandisha kisima kinachofoka maji. Loo, la! Loo, la! Sijali inakuwa baridi jinsi—jinsi gani, haitakigandisha hicho. Utagandisha birika; baridi kali ndogo tu itafanya jambo hilo. Mnaona?

Bali kila kinachosogea, kilicho na Uhai ndani yake, kinasogea huku na huko. Nawe huwezi kugandisha Kisima kinachofoka maji. Hata roho iliyo mahali pale iwe ni ya huzuni namna gani, Kisima hiki daima ni hai. Ishi kwenye Kisima hicho.

¹³⁷ Nami niliona pale, nilipita pale na ningekinywea, na, loo, jamani, maji matamu tu! Hukujisumbua hata kidogo, “Sijui, kama nikifika pale, sijui kama kimekoma kufoka tena?” Kimekuwa kikifoka . . .

¹³⁸ Mzee mkulima aliniambia, kasema, “Babu yangu alikinywea.” Kisha kasema, “Hakijapungua kamwe ama cho chote kile. Kingali ni kisima kile kile, kinachuruzikia kwenye Mto Blue kule.”

¹³⁹ Nikawaza, “Loo, jamani, ni mahali pazuri jinsi gani pa kunywea maji!” Ningetembea kadiri ya maili moja kutoka njiani, kufikia mahali pale, kwa maana palikuwa mahali pazuri sana pa kunywea maji. Loo, jinsi hayo maji yalivyokuwa mazuri! Loo, jamani!

Ninge—ningeenda kule jangwani, Arizona sasa, ningali nikiwazia, “Kisima kile cha ajabu kule chini, laiti ningejilaza chini kule!”

Kama alivyosema Daudi wakati mmoja, “Loo, laiti ningalinywea kile kisima mara moja tena!” Laiti angalifika tu kule!

¹⁴⁰ Ndipo nikaketi chini siku moja, na kitu fulani cha ajabu kikanipata. Nami nikasema, “Kitu gani kinakufanya ufurahi sana kila wakati? Laiti ningalikuwa na furaha namna hiyo. Mbona, kamwe sijakuona una huzuni, tangu nianze kuja hapa. Hakuna hata jambo moja la huzuni kwako.” Nikasema, “Wewe daima umejawa na furaha. Unarukaruka na kububujika na kupiga makelele. Kipupwe kwa kiangazi, baridi ama joto, hata iwe nini, daima umejawa na furaha. Kitu gani kinakufanya hivyo? Nini, ni kitu gani? Kwa sababu ninakunywa maji yako?”

“La.”

Nasema, “Vema, labda sungura wanakunywea, nawe unapendezwa sana na jambo hilo.”

“La.”

Nikasema, “Vema, ni nini kinakufanya kububujika namna hiyo? Ni kitu gani kinakufanya ufurahi namna hiyo? Ni kitu gani kinakufanya daima ujawe na furaha sana?” Kasema, “Ni kwa sababu—kwamba—kwamba ndege hukunywea?”

“La.”

“Kwa sababu mimi ninakunywea?”

“La.”

Nikasema, “Vema, ni kitu gani kinakufanya ujawe na furaha namna hiyo?”

¹⁴¹ Na kama kisima hicho kingaliweza kunijibu, kingesema hivi. “Ndugu Branham, si kwa sababu unakunywa; ninathamini jambo hilo, na kwa kuwa naweza kuwaridhisha ndege. Namridhisha kila anayetaka kunywa. Jambo tu likupasalo kufanya ni kuja hapa na kunywa. Bali, kinachonifurahisha, si mimi kububujika, ni kitu fulani kilicho ndani yangu, kinanisukuma. Ni kitu fulani kinachonibubujisha.”

¹⁴² Na hivyo ndivyo ilivyo kwa maisha yaliyojazwa Roho. Kama alivyosema Yesu, Yeye alikuwemo ndani, anakupa visima vya maji vikibubujika Uzima wa milele, kisima kinachofoka maji, maji yanayochuruzika ambayo daima yanatiririka. Kama wengine kanisani wametiwa moyo ama wamevunjwa moyo, wewe ungali bado uko Kisimani.

Kwa nini uchukue taratibu ya kale ya kimadhehebu na birika, vilivyojawa na vimelea na kila kitu kinginecho, na kunywea kitu hicho chenye maji yaliyooza, ambapo huku umealikwa kwenye Chemchemi, Kisima kinachofoka maji?

¹⁴³ Nafikiria jinsi kilivyosukuma tu, na kurusharusha, na—na kuchemka, na kucheka, na kufurahi, na kuruka, na kucheza. Kwenye baridi, mvua; joto, kukavu, wakati kwingine kote nchini kulikuwa kunashikwa na ukame, kilikuwa kikibubujika kama kilivyofanya daima. Maana kilikuwa na kina kirefu, imara, kilitoka kule chini kabisa miambani.

¹⁴⁴ Loo, hebu niishi karibu na Chemchemi hiyo! Chukua taratibu zako zote za kujitengezea unazotaka, visima vyako vyote vya kale vya maji yanayooza, lakini hebu mimi nije kwenye . . . ama mabirika yenye maji yaliyooza. Bali, hebu mimi nije kwenye Chemchemi hii, hebu nije pale ambapo Yeye amejaa kabisa. Yeye ndiye furaha yangu. Yeye ndiye Nuru yangu. Yeye ni—Yeye ni nguvu zangu. Yeye ni Maji yangu. Yeye ni Uzima wangu. Yeye ni Mponya wangu. Yeye ni Mwokozi wangu. Yeye ni Mfalme wangu. Kila ninachohitaji kinapatikana Kwake. Kwa nini niwe na hamu ya kukiendea kitu kingine?

¹⁴⁵ Ndugu, dada, mbona usije kwenye Chemchemi hii usiku wa leo? Mbona, iwapo hujawahi kuwepo pale, mbona usiipokee usiku wa leo huku tunapoviinamisha vichwa vyetu?

146 Mabirika yavujayo, yanamwaga, yanapenyeza, ulimwengu ukipenya mle ndani, vinyaa kutoka kwenye maghala ya nafaka na vya kutoka nyakati zingine. Mbona isiwe ni Kisima hiki, ambacho upuzi huo hauwezi kukaa mle, Chemchemi hii kuu iliyojawa na Damu, iliyotoka katika mishipa ya Imanueli? Mbona usiipokee hiyo usiku wa leo? Mungu na atusaidie usiku wa leo, katika nchi hii iliyokauka na yenye kiu. Kama alivyosema nabii, “Yeye ni Mwamba katika nchi ya uchovu.” Yeye ndiye ile Chemchemi. Mbona msije Kwake usiku wa leo, katika mioyo yenu, tunapoomba?

147 Baba yetu mpendwa wa Mbinguni, hakuna Chemchemi nyingine, wakati muziki unacheza, sijui chemchemi nyingine, ila Damu Yake Yesu. Nilizaliwa mle, nimelelewa mle; nataka kuishi mle, na kufia mle, na kufufuka tena mle, katika Uwepo Wake. Sikuzote, Bwana, jalia niwe katika Uwepo Wake, kwa sababu sijui mwingine. Hakuna kanuni ya imani, hakuna upendo; hakuna upendo ila Kristo, hakuna kanuni ya imani ila Kristo, hakuna kitabu ila Biblia, hakuna kitu kingine, hakuna furaha nje Yake. Kumtoa kwangu, Ee Mungu, sijali nimemiliki ulimwengu kiasi gani, i—ingekuwa mauti, ningezunguka kila mahali huku nimeweka mikono yangu juu ya kichwa changu. Kumtoa kwangu, ningega dunia, Bwana. Bali hebu na awe ndani yangu, ndipo Desemba itakuwa tamu kama Mei, ndipo hakuna mahali penye joto na hakuna mahali pakavu, hata mauti yenyewe hayana ushindi. Hebu na tumpate, Baba. Mtoe, kwa wingi, kwa kila mwamini hapa usiku wa leo, kwa kuwa wamengoja katika chumba hiki.

148 Wengi wao hawana budi kuendesha magari barabarani usiku wa leo, wanapoenda makwao, jalia basi wawe wakiwazia jambo hili, “Mimi ninaishi kwenye ile Chemchemi. Ninaishi hapo, nikinywa maji upya, saa baada ya saa.”

149 Na iwapo hawajaipokea hiyo, bado, jalia wampokee sasa, kusudi waondoke waende pamoja na ile Chemchemi. “Nitaambatana nanyi; nitakuwa pamoja nanyi hata ukamilifu wa dahari.” Yajalie mambo haya, Baba.

150 Na sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa, kuna mtu humu ndani, usiku wa leo, ama ni wangapi wangesema, “Bwana, nipeleke kwenye chemichemi hiyo sasa hivi. Sijakuja hapa kusikia tu; naja hapa kutafuta Kitu fulani. Naja hapa kukutafuta Wewe, Bwana. Nina haja Nawe usiku wa leo. Njoo moyoni mwangu sasa hivi. Utafanya hivyo, Bwana?” Mungu awabariki. Bwana ambariki kila mmoja.

151 Baba, unaiona mikono, imeinuliwa kila mahali hata ukutani, na katika vyumba vingine, huko nje. U—umeiona, Baba. Na—naomba ya kwamba utawatimizia haja zao zote. Labda wamekuwa wakinywea birika fulani la kale, Bwana, kituo fulani cha katikati ambapo mtu fulani alichimba birika, limekwisha

kuambukizwa na namna zote za mafundisho ya kigeni, likikana Neno. Naomba, Mungu, ya kwamba usiku wa leo watamjia Yeye Ambaye ndiye Chemchemi ile, Chemchemi ile ya Uzima. Tujalie, Baba. Nawakabidhi Kwako sasa katika Jina la Yesu.

¹⁵² Nawe uliniambia, “Ukiomba lo lote katika Jina Langu, litatimizwa.” Sasa, nisingeomba jambo hili, Bwana, kama sikufikiria lingetendwa. Ninge—ningekuwa nikilisema kwa utaratibu wa dini. Bali nawaombea, kwa uaminifu. Nawaombea, nikiamini ya kwamba utatujalia uliyoahidi.

¹⁵³ Na sasa nawatoa kwenye lile birika usiku wa leo. Nawatoa mahali walipokuwa wakinywea, mahali ambapo hawaridhiki; hadi kwenye hii Chemchemi. Nafanya hivyo katika Jina la Yesu Kristo.

¹⁵⁴ Wao ni Wako, Bwana. Hebu na wanywee Kwako, Maji yaliyo hai, Chemchemi ya Maji yaliyo hai. Katika Jina la Yesu, naomba. Amina. Tujalie, Bwana.

Hakuna kabisa
Dawa ya makosa
Ya kututakasa.
Ila Damu Yake Yesu.
Sioshwi dhambi zangu,
Bila Damu Yake Yesu.
Hapendezewi Mungu,
Bila Damu Yake Yesu . . .

Ee Yesu, waponye hawa, Bwana! Tujalie, Bwana, katika Jina la Yesu. Naomba, Mungu, ya kwamba Wewe . . . ? . . . Unayajua mambo yote.

Ya kututakasa,
Loo, Ila Damu . . .

¹⁵⁵ Liwazie jambo hilo, sijui chemchemi nyingine! Sijui kitu kingine ila Yeye. Sitamani kujua kitu ila Yeye. Ni Damu ya Yesu tu! Loo!

Hakuna kabisa
Dawa ya makosa
Ya kututakasa.
Loo, ila Damu Yake Yesu.

¹⁵⁶ Tunapouimba huo tena, hebu na tupeane mikono mmoja kwa mwingine. Je! mnapendana? Kuna mtu hapa aliye na neno dhidi ya mwingine. Kama yupo, nenda kaliweke sawa, tafadhali. Hebu tusiondoke hapa namna hiyo. Mnaona? Kama una neno juu ya mtu ye yote, nenda ukaliweke sawa, sasa hivi. Huu sasa ndio wakati wako wa kwenda kule, na kusema, “Ndugu, dada, nilisema neno dhidi yako, niliwaza neno. Sikutaka kufanya hivyo. Nisamehe.” Mnaona, hiyo ndiyo njia ya kulifanya. Hebu na tuwe na Chemchemi hiyo miongoni mwetu, wakati wote. Unaona?

Ya kututakasa.
Ila Damu Yake Yesu.

Loo, hakuna kabisa
Dawa ya makosa
Loo, ya kututakasa.
Ila Damu Yake Yesu.

¹⁵⁷ Loo, si Yeye ni wa ajabu? Hakuna chemchemi nyingine! Sisi hatutajiambukiza na mambo mengine. Tumejitenga, tukauacha ulimwengu nyuma. Hatutaki tena vitunguu saumu vya Misri na mabirika yavujayo. Tuko safarini na Bwana Yesu, ule Mwamba uliopigwa, amina, tukila Mana itokayo Juu, na tukinywa; tukila Chakula cha malaika, na kuunywea ule Mwamba. Amina!

Yakututakasa,
Ila Damu Yake Yesu.

Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu.

¹⁵⁸ Naomba ya kwamba Mungu atawabariki kwa wingi sana kila mmoja wenu, ya kwamba neema Yake na rehema zitaambatana nanyi katika juma lijalo. Na kama lo lote likitukia, kwamba mmoja wenu apenye aende upande wa pili wa pazia sasa, kumbuka tu ni usingizi na raha ya masaa machache tu hata tutakapokutana. Kumbukeni, ya kwamba, “Hao walio hai na waliosalia hawatawatangulia hao waliokwisha kulala mauti, kwa maana Parapanda ya Mungu, ile Parapanda ya mwisho. . . .” Ya sita tayari imepigwa. Na Parapanda hiyo ya mwisho, kama ile Muhuri ya mwisho, itakuwa Kuja kwa Bwana. “Italia, na hao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza.” Wanastarehe tu hata wakati huo.

¹⁵⁹ Na kama ukijeruhiwa, kumbuka:

Peleka Jina la Yesu
Ko kote uendako;
Utakapojaribiwa,
Lilia Jina hilo.
(Pepo watakimbia.)

¹⁶⁰ Kumbukeni tu, tunatarajia kukutana nanyi hapa Jumapili ijayo asubuhi. Waleteni wagonjwa na wanaoteseka. Nitakuwa nikiwaombea. Nanyi niombeeni sasa. Mtafanya hivyo? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Nitawaombea, ya kwamba Mungu atawambariki.

. . . Jina hilo.

Thamani, thamani, na tamu,
Ni Jina Lake Yesu;
Thamani, na tamu,
Ni Jina Lake Yesu.

Kwa Jina la Bwana Yesu,
Nimejiinamisha;
Ndiye Mfalme wa wafalme,
Hakika ya maisha.

Thamani, na tamu, (si ni tamu na la thamani?)
Ni Jina Lake Yesu;
Thamani, na tamu,
Ni Jina Lake Yesu.

¹⁶¹ Daima ni vigumu sana kuwaacha. Ingawa najua ya kwamba mnaona joto jingi, bali kuna kitu fulani kuhusu... Hebu, kifungu kimoja zaidi, sivyo? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Sivyo? *Kibarikiwe Kifungo Kifungacho*, dada. Wangapi wanaujua huo wimbo wa kale? Tulizoea kuuimba, miaka kadha iliyopita.

¹⁶² Nami nilikuwa nikiwazia, usiku wa leo, "mikono miwili, kati ya mamia ya ambao wamekwisha kuaga dunia," tulipokuwa tukiuumba huo wimbo kwenye Maskani, na kushikana mikono sisi kwa sisi. *Kibarikiwe Kifungo Kifungacho*. Nimewazika wengi wao, papa hapa kwenye makaburi. Wao wanangoja. Nitawaona tena. Mimi huwaona, mara kwa mara, katika ono, wakati ninapoangalia ng'ambo ya pazia. Wako kule.


Hebu na tuviinamisha vichwa vyetu sasa tunapimba.

Kibarikiwe Kifungo Kiifungayo,
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika . . .
Ni kama ule wa Mbingu.

Tutawa . . . (sasa nyosha mkono ukamshike mtu
mwingine mkono) . . . nyikapo,

Sasa inamisha kichwa chako.

Hiyo yatufadhaisha;
Lakini tungali pamoja rohoni,
Hata tutakutanika.

¹⁶³ Huku vichwa vyetu vimeinamishwa. Namwachia mchungaji ibada sasa, na aturuhusu tufumukane kwa maombi. 

MABIRIKA YAVUJAYO SWA64-0726E

(Broken Cisterns)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, tarehe 26 Julai, 1964 katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1992 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org